# DHANA YA MAISHA KATIKA RIWAYA MBILI ZA EUPHRASE KEZILAHABI: KICHWAMAJI NA DUNIA UWANJA WA FUJO

NA

MWANJALA SIMION MWACHOO

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

University of NAIROBI Library
0532197 1

NOVEMBER, 2011

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

Sahihi: ______________________ Tarehe: 4/11/2011.

SIMION MWACHOO MWANJALA

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii tulioteuliwa na chuo kikuu.

Sahihi: ______________________ Tarehe: 11-11-2011

PROF. KYALO WADI WAMITILA, PhD

(Msimamizi)

Sahihi: ______________________ Tarehe: 7/11/2011

DKT. F. MWANGANGI WA MUSYOKA

(Msimamizi)

# TABARUKU

Tasnifu hii nawatabarukia marehemu babangu Johnson Mwanjala na mamangu Jallet Wacheghu walionisomesha na kunifanya niwe na ari ya kutia ghera na kufaulu masomoni.

## SHUKRANI

Kazi hii imetimilika kutokana na ukarimu, juhudi na hisani za watu mbalimbali. Naomba kuwataja baadhi yao kwa misaada, wema na uadilifu wao. Mawazo na ushauri wao uliwezesha kazi hii kufikia kiwango ilichofikia.

Nawatolea shukrani zisizo na kifani wasimamizi wangu Profesa Kyalo W. Wamitila na Dkt. F. Mwangangi wa Musyoka kwa kuniongoza tangu mwanzo hadi tamati ya tasnifu hii. Wao waliniongoza kupitia njia za kweli na za kiusomi.

Ningependa pia kuwashukuru wahadhiri wengine ambao waliniandaa kufikia kuweza kukabili kazi ya kitaalamu kiasi hiki. Hawa ni Profesa John Hamu Habwe (Mwenyekiti wa Idara), Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Kineene wa Mutiso, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Mwenda Mbatiah, Dkt. Jefwa Mweri na mwalimu Basilio Mungania.

Sitamsahau mke wangu mpendwa Christine Walegwa na watoto wangu Jallet Wacheghu, Johnson Mwanjala, Daniel Kichuchu na Dennis Mwanyange. Uvumilivu wao ulinipa moyo wa kusoma kwa bidii na kukamilisha shahada yangu ya uzamili.

Shukrani pia ni kwa wanafunzi wenzangu tulioabiri jahazi hili la masomo pamoja. Hawa ni Peter Mburu, Margaret Too, Angelina Mainga, Reuben Mwilaria, Mwito Mukaria, Alex Kinyua, Joyce Karinge, Joyce Murage, Oluga Owada, Njuguna Samuel , Dadson Ngunjiri, Pamela Tambasi, Josephine Mbula, Howard Muhanda, Lincolin Nyaga, Andrew Watuha, Amos Ngugi, Mary Apopo na Timothy Mukaria.

Pia nawashukuru marafiki zangu Bw. Meshack Pongah, Dishon Mngoda, Benjamin Mwawasi na Gibran Nzaro ambao walinitia shime katika safari yangu ya masomo.

Hatimaye namshukuru Florence Otiende kwa kuichapa kazi hii kwa ustadi. Kwenu nyote nasema ahsante na Jalia awajalie yote mema.

**YALIYOMO**


UNGAMO ..... ii

TABARUKU ..... iii

SHUKRANI ..... iv

YALIYOMO ..... v

MUHTASARI ..... vii

**SURA YA KWANZA ..... 1**

1.1 UTANGULIZI ..... 1

1.2 SOMO LA UTAFITI ..... 1

1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI ..... 2

1.4 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO ..... 3

1.5 UPEO NA MIPAKA YA SOMO ..... 3

1.6 NADHARIA TETE ..... 4

1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI ..... 4

1.8 MSINGI WA KINADHARIA ..... 7

1.9 NJIA ZA UTAFITI ..... 21

**SURA YA PILI ..... 22**

DHAMIRA NA MOTIFU ZA UDHANAISHI KATIKA RIWAYA YA ..... 22

KICHWAMAJI ..... 22

2.0 UTANGULIZI ..... 22

2.1 UKATAJI TAMAA KATIKA RIWAYA YA KICHWAMAJI ..... 22

2.2 UKENGEUSHI KATIKA RIWAYA YA KICHWAMAJI ..... 27

2.3 SUALA LA UTEUZI KATIKA RIWAYA YA KICHWAMAJI ..... 33

2.4 DHAMIRA YA KIFO KATIKA RIWAYA YA KICHWAMAJI ..... 36

2.5 HOFU, KIHORO, DUKUDUKU KATIKA RIWAYA YA KICHWAMAJI.... 39

2.6 MSAKO WA MAANA YA MAISHA KATIKA RIWAYA YA KICHWAMAJI ........................................................................................................ 40

2.7 SUALA LA MUNGU KATIKA RIWAYA YA KICHWAMAJI ..................... 47

2.8 HITIMISHO........................................................................................ 50

**SURA YA TATU ........................................................................................ 51**

DHAMIRA NA MOTIFU ZA UDHANAISHI KATIKA RIWAYA YA DUNIA UWANJA WA FUJO ........................................................................... 51

3.0 UTANGULIZI ...................................................................................... 51

3.1 SUALA LA UTEUZI ............................................................................ 51

3.2 UKENGEUSHI KATIKA DUNIA UWANJA WA FUJO ............................ 64

3.3 KIHORO, HOFU/DUKUDUKU KATIKA RIWAYA YA DUNIA UWANJA 68

WA FUJO ................................................................................................ 68

3.4 UKATAJI TAMAA KATIKA DUNIA UWANJA WA FUJO......................... 72

3.5 DHAMIRA YA KIFO KATIKA RIWAYA YA DUNIA UWANJA WA FUJO ........................................................................................................ 77

3.6 MSAKO WA MAANA YA MAISHA KATIKA RIWAYA YA DUNIA UWANJA WA FUJO ........................................................................... 79

3.7 HITIMISHO........................................................................................ 88

**SURA YA NNE ........................................................................................ 90**

4.1 HITIMISHO WA MAPENDEKEZO ........................................................ 90

4.2 HITIMISHO........................................................................................ 90

4.3 MAPENDEKEZO.................................................................................. 98

MAREJELEO ............................................................................................ 99

# MUHTASARI

Katika tasnifu hii tumechunguza dhana ya maisha katika riwaya mbili za *Euphrase Kezilahabi* ambazo ni *Kichwamaji* na *Dunia Uwanja wa Fujo.*

Uhakiki huu umegawanywa katika *sura nne*. Katika *sura ya kwanza* tumebainisha somo la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu za kuchagua somo, upeo na mipaka ya somo, nadharia tete, yaliyoandikwa kuhusu somo hili, msingi wa kinadharia na njia za utafiti.

*Katika sura ya pili,* tumeonyesha dhana ya maisha katika riwaya ya *Kichwamaji.* Tumevihakiki vipengele/mihimili ya udhanaishi katika riwaya hii,vikiwemo ukengeushi, kutawala kwa suala la uteuzi na wingi wa uteuzi, fujo katika maisha, udhaifu wa maisha ya mwanadamu, upweke na usiri, kihoro na hofu kubwa, utupu na ubwege wa maisha, swala la uhuru, swala la kifo (mauti).

Katika *sura ya tatu,* tumeonyesha dhana ya maisha katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo.* Vilevile, tumevihakiki vipengele/mihimili ya udhanaishi katika riwaya hii.

Katika *sura ya nne,* tumehitimisha kwa kutoa maoni yetu kuhusiana na kazi hii kwa ujumla. Aidha tumetoa maelezo kuhusu mafanikio pamoja na mapendekezo ya utafiti zaidi.

Tumehitimisha kwa kuonyesha marejeleo ya baadhi ya kazi ambazo zimeandikwa kuhusu kazi za Euphrase Kezilahabi na nadharia ya udhanaishi tunazozishughulikia.

# SURA YA KWANZA

## 1.1 UTANGULIZI

Tasnifu hii imeshughulikia dhana ya maisha katika riwaya za Kichwamaji na Dunia Uwanja wa Fujo zilizoandikwa na Euphrase Kezilahabi. Tumejaribu kuonyesha dhana ya maisha inavyodhihirika katika riwaya hizi mbili kwa kuzingatia usawiri wa wahusika.

Katika sura hii, tumebainisha somo la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu za kuchagua somo, upeo na mipaka ya somo, nadharia tete, yaliyoandikwa kuhusu somo hili, msingi wa kinadharia na njia za utafiti.

Mbali na kazi hizi, mwandishi huyu vilevile ameandika riwaya za *Rosa Mistika (1971), Gamba la Nyoka (1988), Nagona (1990) na Mzingile (1991)* vilevile ameandika tamthilia ya *Kaptula la Marx (1999).*

## 1.2 SOMO LA UTAFITI

Tasnifu hii itajishughulisha na uhakiki wa riwaya mbili za Euphrase Kezilahabi, yaani *Kichwamaji (1974)* na *Dunia Uwanja wa Fujo (1975).* Tutachukuwa kila mojawapo ya kazi hizi na kuchunguza dhana ya maisha inavyodhihirika. Tunadhamiria kuchunguza mtazamo wa mwandishi huyu wa maisha huku tukitathmini falsafa yake kuhusu suala la maisha.

Ni vyema kufahamu kuwa, mbali na kukusudiwa kuwa njia ya kukosoa wanyanyasaji katika jamii ya Tanzania mnamo miaka ya sabini, riwaya za *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Kichwamaji* zimenuiwa kuwa chombo cha kuuliza maswali ya kimsingi kuhusu maana ya maisha ya mwanadamu na jamii nzima ya vitu vilivyoumbwa.

Maudhui katika riwaya hizi mbili yamejadiliwa kwa mtazamo wa kifalsafa kama inavyodhihirika katika riwaya zenyewe. Tutachukuwa kila mojawapo ya kazi hizi mbili na kuchunguza kwa umaakini jinsi ambavyo suala la maisha limemulikwa.

## 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Madhumuni ya utafiti huu ni

(i) Kuchunguza uchanaishi katika riwaya hizi mbili. Tutachunguza dhana ya maisha katika riwaya za *Kichwamaji na Dunia uwanja* wa fujo kulingana na Euphrase Kezilahabi.

(ii) Kutathmini mtazamo wa mwandishi kuhusu suala la maisha kama inavyojitokeza katika kazi hizi mbili.

Somo letu ni muhimu kwa vile mwandishi ametumia wahusika ambao wanakatisha tamaa, wamekengeuka, kuna hofu kubwa, kihoro/wasiwasi, kuna vifo kadhaa vinavyotokea, kuna suala la uteuzi wanaofanya wahusika, kuna msako wa maisha miongoni mwa wahusika, suala la kuweko au kutokuweko kwa Mungu, uhuru wa mtu binafsi, uwezo wa mtu wa kujifikiria na kujiamulia na wajibu wa binadamu katika ulimwengu n.k. katika kazi hii, tutabaini bayana majukumu ya wahusika ili waeleweke vyema.

## 1.4 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO

Tumeamua kushughulikia mada hii kwa sababu suala la dhana ya maisha ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Vilevile, ingawa falsafa ya udhanaishi ilianza huko mataifa ya Magharibi, waandishi wa fasihi ya Kiswahili wameathiriwa nayo na wamejihusisha na uandishi wa kazi zinazoegemea falsafa hiyo. Tumechagua kuhakiki riwaya hizi mbili za *Kichwamaji* na *Dunia Uwanja wa Fujo* kwa sababu mwandishi huyu ni mashuhuri katika uandishi wa fasihi ya Kiswahili. Kupitia kwa kazi zake, Kezilahabi amechangia

kikamilifu katika kuendeleza fasihi ya Kiswahili kwa jinsi anavyohusisha masuala ya kifalsafa katika uandishi wake.

Kazi za mwandishi huyu za hapo awali zimeshughulikiwa na wahakiki kadhaa katika viwango mbalimbali. Sisi hapa tunanuia kulipa suala la maisha uzito unaostahili kama inavyodhihirika katika riwaya hizi mbili. Mwandishi wa riwaya hizi amelipa uzito na kutilia maanani suala la maisha. Mambo ambayo mwandishi huyu ameyadhibitisha katika riwaya hizi mbili ni masuala ambayo hayatokei tu katika jamii yake, bali katika jamii nzima ya ulimwengu.

## 1.5 UPEO NA MIPAKA YA SOMO

Kama tulivyotaja hapo awali, tunanuia kujikita katika kazi mbili za *Euphrase Kezilahabi* ambazo ni *Kichwamaji (2008)* na *Dunia Uwanja wa Fujo (2007)*. Riwaya hizi mbili zimeonyesha upeo wa juu wa udhanaishi. Katika riwaya hizi, tunapata taswira ya vile ambavyo mwandishi analitazama suala la maisha. Aidha tumerejelea riwaya ya *Rosa Mistika* ili kutilia mkazo masuala ambayo tumeyashughulikia.

## 1.6 NADHARIA TETE

Utafiti wetu utazingatia nadharia tete zifuatazo;

i) Maisha ya mwanadamu hayana furaha.

ii) Katika kazi zote mbili, kuna dhihirisho kuwa maisha hayana maana.

iii) Kazi hizi mbili zinaonyesha ukataji tamaa.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Mwandishi Euphrase Kezilahabi aliyeandika riwaya hizi mbili anajumuishwa pamoja na waandishi mashuhuri wa baada ya ukoloni na wataalam kama vile Mbatiah (1998), Njogu na Chimerah (1999), na Wamitila (2002). Kezilahabi anatambulika kuwa miongoni mwa wadhanaishi wa fasihi ya Kiswahili waliobobea. Ni vyema kufahamu kuwa, wahakiki mbalimbali wameshughulikia dhana na maana ya maisha katika kazi nyinginezo za mwandishi huyu. Hata hivyo, wataalamu hawajaangalia suala la maana ya maisha katika kazi hizi mbili. Tunadhamiria kulipa uzito suala hili la maisha katika utafiti wetu.

M.M. Mulokozi (1976) katika kuhakiki *Dunia Uwanja wa Fujo*, amechambua maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika riwaya hii. Mulokozi amechambua elimu ya kisasa, jambo ambalo ni la manufaa kwetu japo suala la dhana ya maisha halikuangaliwa kama tunavyokusudia kufanya katika utafiti wetu.

Senkoro (1982) katika kitabu chake *Fasihi* amejadili maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Mhakiki huyu ameendelea kuelezea falsafa ya Kezilahabi kuhusu maisha. Japo kazi yake itatusaidia kuelewa mwelekeo wa mwandishi,

tunagundua hapa kuwa amegusia kwa kiasi kidogo mno; hivyo basi suala la maisha halikuangaziwa vilivyo.

P.M. Musau (1985) amemwangalia *Kezilahabi* kama mwandishi aliyekata tamaa. Ameshughulikia kwa kina maudhui ya kukata tamaa. Riwaya ya *Kichwamaji* na *Dunia Uwanja wa Fujo* ni miongoni mwa kazi alizohakiki Musau. Anaeleza kuwa, duniani ni fujo tupu na mahali pasipo na furaha. Amelipa suala la maisha nafasi ndogo mno. Tunakusudia kuliangalia suala hili kwa undani zaidi. Kupitia kwayo, tumemuelewa zaidi mwandishi huyu na kwa jicho la kifasihi.

Lugano R.S. (1989). Kazi hii ya Lugano inarejelea usawiri wa wahusika wa kike katika kazi za Kezilahabi. Hata hivyo, mhakiki huyu hakutizama dhana ya maisha katika kazi alizochunguza kama tunavyodhamiria kufanya katika uhakiki wetu.

Mayaka G. (1991) ameangazia ukengeushi wa wasomi katika riwaya za Euphrase Kezilahabi. Amechambua riwaya za *Rosa Mistika, Kichwamaji, Dunia Uwanja wa Fujo* na *Gamba la Nyoka* huku akiangalia vile wasomi walivyokengeuka katika kazi hizi. Uchambuzi huu utatufaa katika kuchambulia kazi yetu; japo sisi tunahakiki riwaya ya *Kichwamaji* na *Dunia Uwanja wa Fujo*.

Baru T.W. (1992) amehakiki *Bonde la Wakati* katika riwaya za *Kezilahabi.* Alichunguza riwaya za *Rosa Mistika (1971), Kichwamaji (1974), Dunia Uwanja wa Fujo (1975)* na *Gamba la Njoka (1979).* Katika utafiti wake, anaangalia sababu, na jinsi tofauti za umri inakuwa chanzo cha mikinzano katika jamii na hivyo kusababisha kutengana kwa kizazi

cha vijana na kile cha wazee. Ni kazi ambayo itanufaisha utafiti wetu ingawa alipokuwa anachambua, hakutilia maanani suala la dhana ya maisha kama tunavyonuia kufanya katika utafiti wetu.

Gatare (1993) amelihakiki suala la Dini katika riwaya za Kezilahabi zikiwemo *Kichwamaji* na *Dunia Uwanja wa Fujo*. Japo mhakiki huyu alichambua dini katika riwaya akitumia nadharia ya udhanaishi ambayo pia tutatumia katika uhakiki wetu, hakuchambua suala la dhana ya maisha katika riwaya hizi.

Mbatiah (1998) ameziainisha kazi za Euphrase Kezilahabi katika makundi mawili. Kundi la kwanza likiwa na kazi za kipindi cha kwanza, kazi za miaka ya sabini. Riwaya hizi ni; *Kichwamaji, Rosa Mistika, Dunia Uwanja wa Fujo* na *Gamba la Njoka*. Kundi la pili ambazo ni kazi za miaka ya tisini ni *Nagona na Mzingile*. Katika kazi yake, Mbatiah anashughulikia mawazo makuu anayoyashughulikia *Kezilahabi* na hivyo kunufaisha pakubwa utafiti wetu.

Mungah C.I. (1999) amehakiki dhana ya maisha katika Novela mbili za *Euphrase Kezilahabi,* Nagona na Mzingile. Mhakiki huyu amechunguza mtazamo wa maisha wa *Kezilahabi* huku akitathmini falsafa yake kuhusu suala la maisha. Kazi hii itanufaisha utafiti wetu ingawa wachambuzi hawa hawakutumia nadharia ya udhanaishi kama tutakavyofanya bali walitumia nadharia ya kisosholojia.

Nguku K.A. (2006) amehakiki riwaya ya *Kichwamaji* katika tasnifu yake; udhanaishi na Fumbo la Mungu: Uchanganuzi Linganishi wa *Kichwamaji* (E. Kezilahabi) na *La Peste*

(Albert Camus). Nguku ameangazia jinsi waandishi hawa wameshughulikia maswala ya udhanaishi na Fumbo la Mungu. Uhakiki huu utatoa mchango mkubwa kwa utafiti wetu japo mhakiki huyu hakutizama dhana ya maisha kama tutakavyofanya katika kazi yetu.

Nkonge G.L. (2006) amechambua athari za udhanaishi katika *Kichwamaji* na *Nguvu ya Sala.* Katika kazi hii, Nkonge amechunguza iwapo riwaya hizi zinaweza kuainishwa kama kazi za kidhanaishi. Kwa vile kazi yetu inalenga riwaya ya *Kichwamaji,* kazi ya mhakiki huyu itakuwa na mchango katika kazi yetu japo yeye hakuzingatia dhana ya maisha bali aliangalia udhanaishi kwa ujumla na athari zake katika riwaya hii ya *Kichwamaji.*

Mbali na wengine walioziangalia kazi hizi mbili, bado kumeachwa pengo la kuzibwa. Pengo lenyewe ni kuihakiki dhana ya maisha katika riwaya hizi. Hilo ndilo lengo kuu la tasnifu yetu. Kazi tulizotaja katika sehemu hii zitatusaidia kwa hali moja au nyingine katika kufafanua mada yetu. Ni matumaini yetu kuwa; kwa kutumia nadharia mahususi, tutapiga hatua kubwa zaidi katika kuzihakiki riwaya hizi mbili.

### 1.8 MSINGI WA KINADHARIA

Utafiti wetu utaelekezwa na kuongozwa na nadharia ya udhanaishi. Udhanaishi ni mwelekeo wa kimawazo unaoshikiliwa na wanafalsafa wenye mitizamo na imani tofauti. Ulijikokeza ujerumani miaka michache baada ya vita vikuu vya kwanza na ukaenea hadi *Ufaransa, Italia, Ujerumani* na nchi nyingine. Baadhi ya wanaoshikilia nadharia hii

wanasema kuwa imani ya kuweko kwa Mungu ni dhana ambayo haina msingi wowote. Wengine wanaona kuwa kuweko au kutokuweko kwa Mungu si suala la kuzua mjadala.

Ijapokuwa wananadharia hii wana mitazamo na imani tofauti, kuna sifa mojawapo ambayo ni ya kimsingi. Sifa hii ni kule kujishughulisha na suala la maisha ya binadamu. Wanaudhanaishi humwona binadamu kama kiumbe pweke aliyetupwa katika ulimwengu unaomtesa. Katika kujishughulisha na maisha ya binadamu, wanaudhanaishi hutilia maanani tajriba za mtu binafsi katika safari yake ya maisha.

Japo wanahistoria hutofautiana kuhusu mwasisi wa falsafa hii, inaaminika kuwa nadharia hii iliasisiwa na watu kama St. Augustine, Duns Scotus, na Pascal Blaise.

Kwa muhtasari, ifuatayo ni baadhi mhimili ya nadharia ya udhanaishi;

(i) Waandishi wengi ambao wanajadili kuhusu udhanaishi wanatilia mkazo matatizo halisi yanayomsibu mwanadamu. Wanakwepa imani ya kinjozi juu ya maana ya kuishi.

(ii) Kwao, kwamba Mungu yupo au aliuumba ulimwengu ni suala ambalo hawalishughulikii kwa sababu halioani na mantiki na fikra zao.

(iii) Baadhi ya maudhui yanayotajwa na wadhanaishi ni kama vile; uhuru wa mtu binafsi, uwezo wa mtu wa kujifikiria na kujiamulia na wajibu wa binadamu katika ulimwengu. Kwa vile mwanadamu angekuwa chochote, ubinafsi ni muhimu kwa sababu jukumu la kujitekelezea na kujiridhisha, ni la kibinafsi.

(iv) Maudhui mengine yaliyotagaa katika udhanaishi ni ukengeushi; hali ya kutokuwa na uhakika (chochote chaweza kutokea), kukata tamaa na mauti. Hata hivyo kuna wadhanaishi wanaosawiri tumaini fulani.

(v) Ugwe unaowaunganisha wadhanaishi wote, wenye kukata tamaa kwa wenye kutumaini ni kwamba wanahisi na huzungumzia kwa hamasa tanzia iliyokurubiana na maisha ya binadamu. Wanaonyesha kwamba juhudi za mtu za kujitafutia maana ya maisha mara nyingi huishia katika mauti. Mwisho wa mwanadamu ni kifo. Mchango wa udhanaishi unahusiana na uwezo wake wa kuitalii maisha ya binadamu kihisia na kinafsia.

(vi) Pamoja na haya, udhanaishi unajadili hali kama vile fadhaa, mashaka n.k. na jinsi zinavyoathiri maisha ya binadamu.

Ni muhimu kutaja kwamba katika utafiti huu si mihimili yote tutakayotumia. Itakayotumika ni ile itakayofaa zaidi kufafanua riwaya tunazochunguza ili kuweza kuangaza dhana ya maisha.

*Cassell's Encyclopedia of World Literature (1953: 213)* imefasili *udhanaishi* kuwa kuna makundi kadhaa ya kifalsafa ambayo yapo chini ya udhanaishi. Makundi haya husisitiza udhabiti wa tajriba ya mwanadamu na uhai wake kinyume na nadharia zisizo na mashiko za kuwazika watu. Uk. 224 inafafanua kuwa chini ya mada ya udhanaishi kumewekwa makundi ya kanuni za kifalsafa ambazo zote husisitiza kuwako kwa mwanadamu akiwa na tajriba na umoja.

Ni bayana kuwa hii ni nadharia inayojikita katika falsafa inayoangalia binadamu kama kiumbe maalum na chenye upekee, ambacho kimejitenga na kimetupwa katika ulimwengu katili na usiomjali. Mwanadamu ana uwezo na uhuru wa kufanya uchaguzi anaotaka na hivyo kuamua hatima yake.

*A Dictionary of Literary Terms (1977: 148)* inaeleza kuwa udhanaishi ni neno lililo na maana tofautitofauti lakini linajumuishwa katika maandishi yanayosisitiza uwajibikaji wa mwanadamu kufanya maamuzi yake mwenyewe, uhuru na malengo yake binafsi. Udhanaishi unasisitiza kuwa mwanadamu anajiwajibikia mwenyewe kwa sababu ana hiari ya kufanya atakavyo. *(1977: 251),* inaeleza kuwa *udhanaishi* huegemea katika maoni ya hali ya maisha ya mwanadamu, mahali pake na vilevile jukumu lake, mahusiano yake au ukosefu wa mahusiano yake na Mungu.

*Encyclopaedia Americana (1977: 762)* inafafanua kuwa, *udhanaishi* ni nadharia ambayo huhusisha mitindo na imani mbalimbali na kati ya sifa za kimsingi inayoelezwa ni asili ya ulimwengu na vile ulimwengu huu unavyojishughulisha na kuwepo kwa mwanadamu. Hukataa dhana zenye misingi ya kijamii inayodunisha kuwepo kwa mwanadamu ulimwenguni na kukubali uhuru wake. Vilevile, huwasilisha maasi dhidi ya mawazo na asasi ambazo hupinga uwajibikaji na kuzuia uhuru wa binadamu.

*Oxord Advanced Learners Dictionary (1989: 420)* inafafanua kuwa *udhanaishi* ni nadharia ambayo inamrejelea mwanadamu kama kiumbe aliye na uhuru na anawajibika kwa matendo yake katika dunia isiyo na maana. Maelezo haya yanasisitiza wazo la kuweko kwa binadamu ulimwenguni.

Wafula na Njogu (1999) wanafafanua kuwa udhanaishi ni falsafa kuhusu dhana ya maisha. Istilahi inayotokana na neno "kutamauka". Kutamauka ni kutokuwa na furaha kwa kujua na kuhisi kwamba hakuna tumaini katika maisha namna yalivyo.

K. Njogu na R. Chimerah (1999).Wanaeleza kuwa nadharia ya udhanaishi inajishughulisha zaidi na dhana ya maisha. Maisha ni nini? Wadhanaishi huchunguza kwa undani nafasi ya binadamu ulimwenguni. Pia, wanajihusisha na uchunguzi kuhusu uhusiano wa binadamu na Mungu. Hii ni nadharia iliyoshika sana katika mataifa ya kimagharibi wakati wa vita vikuu vya dunia na baadaye. Nyakati hizo, maisha yalionekana kutokuwa na maana hasa kwa ajili ya kijamii. Watu wengi walihisi kutokuwa na matumaini maishani.

Udhanaishi ni falsafa inayoshughulikia maswala kuhusu "maisha". Ni mtazamo unaokagua kwa upembuzi hali na nafasi ya mtu katika ulimwengu anaoishi. Pia, ni falsafa inayozungumzia uhusiano uliopo kati ya mtu na Mungu; na iwapo mtu anapaswa kuamini kuwepo kwa Mungu.

Wamitila K.W. (2003). Anaeleza kuwa udhanaishi ni dhana inayotumiwa kueleza falsafa ya kuwako au maisha. Dhana hii inatumiwa kueleza maono au mtazamo unaohusiana na hali ya maisha ya binadamu, nafasi na jukumu lake ulimwenguni na uhusiano wake na Mungu.

Wamitila (2003: 248 – 249) ameorodhesha sifa za udhanaishi kama vile ukengeushi. Anafafanua kuwa, kwa mujibu wa wafuasi wa mtazamo huu, maendeleo ya kisayansi na ya kitaswira yamemkengeusha binadamu kutoka kwa Mungu, jamii na kutoka kwa nafsi yake. Dukuduku au kihoro kikubwa (anxiety), ukano au kutokuwepo kwa kitu (nothingness) chenye maana na uhuru ni baadhi ya masuala yanayohusishwa na wanaudhanaishi.

Uhuru, kama anavyofafanua Wamitila, ni kwamba binadamu ana uhuru mkubwa wa kuchagua chochote na kuwa chochote. Anakabiliwa na upana mkubwa unaoishia kuwa wa kutisha na unaoweza kumletea uwazi fulani. Dukuduku au kihoro kikubwa (anxiety) kwa maoni ya wanaudhanaishi ni kiumbe ambaye amekengeushwa na nafsi yake, na anajikuta katika umati mkubwa na alazimikaye kufanya uteuzi fulani, anaishia katika hali ya dukuduku. Suala hili linajitokeza katika kitabu cha Kierkegaard kiitwacho *Fear and Trembling*.

Tuki: *Eng-Swahili Dictionary (2006)* wanaeleza kwamba, *udhanaishi* ni falsafa inayokiri kwamba dunia haina mantiki na binadamu yu huru kuchagua mwenyewe na anawajibika kwa vitendo vyake.

Onyango C. F (1993) katika tasnifu yake; *The Agnostic Implication of Jean – Paul Sartres Philosophy* – anaeleza kuwa istilahi hii iliundwa na Jean Paul Sartre. Inahusu msururu wa wanafalsafa miongoni mwao wakiwemo Martin Heidegger, Karl Peter, Gabriel Marcel na Sartre.

Sőren Kierkegaard ndiye aliyekuwa mtangulizi wa nadharia hii. Wanafalsafa hawa walikuwa na hamu ya kumtambua mwanadamu kama kiumbe ambaye kwa sababu ya uhuru na ubunifu alionao kuonyesha umaarufu dhidi ya viumbe wengine. Pili, jambo kuu linalojishughulisha na nadharia hii ni uthabiti wa kuwako kwa mwanadamu. Wanaudhanaishi wanapendelea kuelezea data ya kuwako Kisahihi.

Sőren Kierkegaard (1813 – 1855) ndiye aliyeboresha nadharia hii. Katika vitabu vyake kama *Sickness Unto Death*, *Fear and Trembling* na *The Concept of Dread* vilisaidia sana katika kutoa na kukuza msingi bora na imara wa nadharia hii. Kierkegaard alieleza kuwa mwanadamu hupata kimbilio kutoka mivutano ya maisha kupitia kwa Mungu. Hii ni imani ambayo iliishia kushika nguvu sana katika Ukristo (Christian Existentialism).

*Shaw, H. (1972; 148).* Maelezo yake yanaafikiana kwa karibu na yale ya *Encyclopedia Americana* (1977: 762) kuwa Kierkegaard, Mwanatheolojia wa *Ki-Deni* aliyejitahidi sana kuendeleza udhanaishi. Yeye anaweza kuelezwa kama mwanzilishi wa udhanaishi wa kisasa. Hata hivyo, mwanafalsafa huyu anapaswa kumtambua mwanafalsafa wa Kifaransa ambaye pia alikuwa mwandishi wa riwaya *Jean-Paul Sartre* ambaye alitamka "Mwanadamu yuko pekee katika ulimwengu usio na Mungu". Sartre, pamoja na wafuasi wake wa baada ya vita vya pili vya dunia wanasisitiza kuwa ulimwengu hauna maana, dhana inayoleta kihoro, upweke, aibu/soni na ukataji tamaa.

Udhanaishi wa Sartre kama ule wa Albert Camus, Simone de Beauvoir, Samuel Beckett, na Franz Kafka, ni wa ukanaji Mungu (atheistic existentialism) lakini wenye muundo wa udhanaishi wa kikristo (Christian exiswtentialism).

Makundi yote mawili ya udhanaishi;

(i) Yanajishughulisha na hali ya kuwako kwa mwanadamu na ulimwengu.

(ii) Yameshawishika kuwa fikira na akili haitoshi kuelewana kuvumiliana na fumbo la kuishi.

(iii) Yanafahamu kuwa maumivu na kukata tama ni kawaida kwa kila mtu.

(iv) Yanakaza imani kuwa uadilifu unategemea mtazamo chanya na kushiriki kikamilifu katika maisha.

Barret W, (1958: 102). Katika *kitabu* hiki, *Barret* anaeleza kuwa, wadhanaishi wa kisasa wamesisitiza kuwa kuweko ni muhimu kuliko hali ya kuwako. Mwanadamu anaishi na anajitahidi kuwa vile alivyo. Hali yake ya kibinafsi ya hali ya kuwako au kilimwengu inatokana na kuweko kwake na kwa fasihi hii ni sawa kusema kuwa kuweko ni muhimu kuliko hali ya kuwako.

(1958: 150) Barret anazidi kufafanua kuwa, Sőren Kierkegaard alikuwa na hisia kali kwa ukristo. Lakini sanasana alijishughulisha na maana yake. Shida ya Kierkegaard; asema Barret ni kwamba alichagua Ukristo. Kila wakati alijipa moyo kwa nguvu zake zote.

Morris, Van Cleve *(1966:11 – 15)* Vilevile anakubaliana na dhana kuwa kuweko (Existence) ni muhimu kuliko hali ya kuwako (essence) "Existence Precedes Essence" kulingana na Morris, mjadala huu unanuiwa kufafanua kuwa, kiasi kuweko kwetu si kwa kubahatisha, hali ya kuwako inamtegemea mwanadamu mwenyewe. Hata hivyo kuna baadhi ya watu ambao hawawezi kufanya maamuzi wenyewe; wanataka mtu awashauri jinsi ya kufanya, jinsi ya kuamini, na jinsi wanatakiwa kukaa au mwelekeo watakaofuata.

Baldick C *(1990: 89)* Baldick. Anakubaliana na maoni ya waandishi watangulizi kuwa *Sőren Kierkegaard* katika miaka ya 1840's alijulikana na kutambuliwa kama aliyeanzisha upya nadharia hii lakini katikati ya karne ya 20 habari hizi zilienea Ufaransa na Ujerumani. Anaeleza kuwa wanafalsafa wa Kijerumani Martin Heidegger na Karl Jaspers waliwajibika sana miaka ya 1920's na 1930's kwa kazi zaidi ya manufaa ya Jean Paul

Sartre na wanaudhanaishi wengine wa Kifaransa wakiwemo Simone de Beauvour, Albert Camus na Maurice Merleau Ponty.

*Encyclopedia Britanica* (1958: 5) inaeleza kuwa, jamii ya wanafalsafa tangu miaka ya 1930 wamejitolea kwa fasiri ya kuweko kwa mwanadamu duniani ambayo inasisitiza uthabiti na silika mbaya. Kwa hivyo, kuweko inajumuishwa kama maalum na kibinafsi inayotupa maana ya kiumbe; Binadamu.

Blackhan, H.J. (1961: 138), Anaeleza kuwa Kierkegaard ndiye asili/chanzo cha udhanaishi kuwa Mungu ni, lakini haishi. Kuweko hakuwezi kutabiriwa kuwa wa milele, kiumbe asiyebadilika kwa vile kuweko kuna maana ya kujishughulisha na kuwa muda, uhuru na historia. Mwanadamu si karibu na kuweko, lakini yeye ndiye kiumbe wa kweli aliyeko.

Warnock, M. (1970: 7) Anatueleza kuwa Kerkegaard mwenyewe alimuiga Socrates ambaye hakuwa na lengo lolote bali kupotosha watu tu. Wale ambao walifundishwa nao, waligundua kuwa kujifunza kwa wapotofu hawa kulikuwa uwongo (1970: 12). Warnock anakariri kuwa Kierkegaard ndiye aliyekuwa mwasisi wa udhanaishi. Hii ni kwa sababu utiifu wa udhabiti wa ukweli pamoja ndio umaakini. Yeyote yule ambaye ametawaliwa na sayansi kimaadili amechelewa na anahitaji kuokolewa kutoka hali yake ya kuwa gizani. Mwanadamu ambaye amebadili dini anaonyeshwa kuwa yu huru. Jambo la kwanza yuko huru kuchagua kama atasogea kutoka daraja moja hadi lingine. Ni katika hali hii ambapo Kierkegaard mtu wa imani yuko huru. Yeye anajitawala kibinafsi. Zaidi ya hivyo, yeye ni mbunifu.

Pojman, Louis P. (1976: 27). Katika tasnifu yake ya *PhD, Pojman* anamnukuu Kierkegaard katika kitabu chake cha *Fear and Trembling* kuwa; sheria inayotumika ulimwenguni inamwambia Ibrahamu asiuwe, kuwa atunze uzao wake, lakini Ibrahamu anasikia sauti nyingine ambayo anaitambua kuwa ya Mungu ikimuagiza amtoe kafara mwanawe Isaka. Vilevile, sheria ya kilimwengu ni ya kila mwanadamu awe na akuze familia yake lakini Kierkegaard anaona kuwa ana wito wa kumtumikia Mungu na mwanadamu kama mjane, hana hiari ya kutotii sheria hii.

Mwanadamu aliyesikia au kutambua sauti ya Mungu kuwa ya kipekee ni sharti aishi kwa uoga na kutetema *(Fear and Trembling)* kwa sababu hawezi kuwa na uhakika kuwa hajajidanganya katika upweke wa kuweko nje ya ulimwengu.

Katika kazi zake mbalimbali, Kierkegaard alijitahidi kuuliza maswali kama: "Maisha ya binadamu yana maana gain?" na "Je, kuna lengo gain katika maisha ya binadamu?" Mwanafalsafa huyu alimwona binadamu kama kiumbe anayeteseka na anayeishi katika ulimwengu usiomjali, aliyezungukwa na mateso na ubwege na anayeshindwa kukabiliana au kupatana vyema na uhalisi huo. Kwa mujibu wa mwanafalsafa huyu, inakuwa vigumu kuyakinisha kuwako au kutokuwako kwa Mungu kwa kuwa maarifa aliyo nayo binadamu yana kikomo. Hali ya kuyatafuta maarifa inabakia kama msukumo mkuu wa maisha ya binadamu. Baada ya Kierkegaard, udhanaishi ulipata msukumo mpya katika karne ya ishirini kutokana na mawazo ya Friedrich Nietzsche, Martin Heidegger, na Karl Jaspers.

Sifa mojawapo muhimu katika mtazamo huu ni imani kuwa "kuweko": (existence) ni muhimu kuliko "hali ya kuwako" (essence). Kinyume chake ndicho kilichosisitizwa katika mikabala ya kijadi ya kifalsafa, yaani hali ya kuwako ni muhimu kuliko kuwako

kwenyewe. Nietzsche anaeleza pia kuwa, hamna ukweli wa kimaadili au wa kisayansi unaoyaongoza maisha ya binadamu. Binadamu kama kiumbe, kwa hivyo, anaongozwa na "usorazini" (Irrationalism). Ikiwa hakuna ukweli wa kimaadili, basi inakuwa vigumu kuongea juu ya ukamilifu wa "wema" au "ubaya". Kwa maoni yake, harakati za Ukristo za kushikilia wema kuushinda ubaya hazifai na zinazaa "hali ya kiutumwa" kwa kuzuia kujieleza huru kwa hisia zilizobanwa.

Friedrich Nietzsche anasifika hasa kupitia kwa kitabu chake *Thus Spake Zarathustra* na *The Will to Power*. Nietzsche alidai kuwa kanisa ni "kaburi la Mungu". Madai haya yanaungwa mkono na Roubiczek (1964: 41) *Existentialism for and Against* kuanzia 1964: 39 – 40, Roubiczek anaeleza matamishi ya Nietzsche kuwa "Mungu amekufa", tumemuuwa Mungu n.k. Kulingana na Roubiczek, hii si kauli ya mkana Mungu aliyeko wazi. Mkanaji Mungu huyu angesema "Hakuna Mungu". Hii ni kwa sababu, msemo "Mungu amekufa" inahusu upotofu wa imani.

Martin Heidegger alikuwa mwanaudhanaishi wa imani ya kwamba binadamu ni mnyonge na hana hiari na matukio ambayo anashuhudia maishani mwake. Kulingana naye, matukio haya hutokea kama ajali maishani mwake; jambo hili halijamfurahisha na kumridhisha binadamu na hivyo kupelekea kujitahidi kuliondoa wazo hili mawazoni mwake, lakini hajawahi kufanikiwa.

Warnock, M. (1970) anaeleza kuwa Heidegger alichaguwa dhamiri. Alichaguwa dhamiri kwa sababu ya mapendekezo ya kiuadilifu. Yeye anapendekeza kwamba binadamu anajifahamu kama kiumbe anayehusishwa na matukio yake ya kale na vile

inavyodhihirika katika maisha yake ya usoni anayochaguwa, ambapo atawajibika maishani mwake na kugunduwa kuwa chaguo alilolifanya ni lake na sio kuongozwa na vile watu kwa ujumla wanavyofanya au kutarajia. Dhamiri basi, itamuonyesha umuhimu wa matendo yake kama sehemu ya njia yake ya kipekee ya maisha aliyochaguwa. Analosisitiza Warnock, hapa ni kuwa, juhudi za binadamu huwa bure kwani mwishoni, mtu hana budi kukosa kile ambacho amekidhamiria.

Heinemann F.H. *(1958: 91 – 92)* ameorodhesha mambo ambayo Hiedegger atakumbukwa kwayo, kama ifuatavyo; Kwanza, alisisitiza kuhusu kuwako kwa mwanadamu, anatilia maanani kuwa, kuweko ni muhimu kuliko hali ya kuwako.
Pili, mwanadamu alipewa heshima na nafasi ya kwanza na muhimu ikilinganishwa na viumbe wale wengine waliohai na wasiohai.

Tatu, kuwako hapa inaeleweka kama kiumbe mwenye nguvu, mtawala (Potential being). Nne, kuwako kwa binadamu ni kiumbe kuwa akiwepo duniani (being-in-the world). Tano, uhusiano wa karibu baina ya kuwako kiumbe na wakati inafaa kuangaliwa.

Wanathiolojia wengine waliojitokeza ni Jean Paul Satre, Albert Comus, Dostoevisky (Notes from underground), Franz kafka na Gerogas Boteuille. Hawa walijitahidi vilivyo kuusambaza udhanaishi.

Kulingana na Sartre, mtu kwanza huchipuka na kuhisi kwamba anaishi kisha mambo mengine yakamfungukia katika hali yake ya kuishi. Kwa mujibu wa maelezo yake, mtu huzaliwa au hujipata ametumbukia kwenye ombwe la aina fulani. Ana uhuru wa

kukaa katika ombwe hilo na kuishi maisha ya utulivu na kukabiliana vilivyo na ulimwengu uliomzunguka. Kwa kuwa hana uwezo juu ya maswala kama vile maumivu na mateso, anaweza kukata tamaa. Hata hivyo, kabla ya kukumbwa na mauti, mtu huyo atafanya matendo yanayoleta maana juu ya maisha yake.

Kuna matapo mawili ya nadharia hi ya udhanaishi;

Tapo moja ni lile ambalo linaongozwa na mkabala wa kilimwengu au wa ukanaji Mungu (Atheist Existentialism). Tapo hili lilichochewa na kuendelezwa na wanafalsafa kama Jean-Paul Sartre, Georges Bataille, Simone de Beauvoir, Maurice Mertean – Purity *Samuel Becket.* Wenye kuunga mkono tapo hili hususan hutilia shaka swala la Mungu. Mwanafalsafa wa kilimwengu Jean Paul Sartre ndiye anayesifika kama kiongozi wa udhanaishi wa kilimwengu.

Tapo la pili ni lile ambalo hufuata mkabala wa Kikristo (Christian Existentialism). Mwanafalsafa Gabriel Marcel ndiye kiongozi wa udhanaishi wa Kikristo. Aliungwa mkono na Heinemann F.H. katika kitabu chake *Existentialism and the Modern Predicament 1958: 218* na kumtaja kuwa yeye ndiye mwanafalsafa maarufu katika tapo hili. Kulingana na Greene N.N. (1960: 61), Gabriel Marcel anatambulika kama kiongozi wa udhanaishi wa Kikristo.

Greene N.N. (1960: 9 – 10) katika Kukariri suala la binadamu na maisha yake magumu katika ulimwengu katili, anaeleza kuwa kuteseka na kuhisi maumivu kwa binadamu ni hali ambayo haiwezi kuepukika ulimwenguni. Inambidi binadamu ayaishi maisha jinsi yalivyo, bila kukwepa. Binadamu amejikuta tu katika hali fulani na ijapo hakuamua

kufuata mkondo wa hali hiyo, analazimika kushikamana nayo kwa sababu hana uwezo kutengana nayo wala kujinasua.

Foulquie, P. (1947: 60) katika kitabu chake Existentialism anakariri kuwa udhanaishi wa Kikristo ndio uliokuwa mkongwe ukilinganishwa na udhanaishi wa kilimwengu. Hata hivyo, udhanaishi wa kilimwengu ndio ambao umeenea sana ukiongozwa na Jean-Paul Sartre. Kuhusu suala la kifo, ambacho ni muktadha muhimu katika nadharia hii, kifo huchukuliwa kama hali ya kawaida na ni daraja nyingine ya maisha. Hapaonekani tofuati baina ya kuishi na kufa.

Gabriel Marcel anajiliwaza kwa dhana ya kwamba kifo ni mwanzo tu wa maisha ya milele.

Mwanafalsafa Samuel Beckett (1964) anadai kwamba, maisha ni kuendelea kufa; kwamba maisha ni kifo cha polepole. Maisha yanaonekana kama kitendawili ambacho binadamu anapaswa kukitegua. Iwapo atafaulu kukitegua basi, mwanadamu atakuwa amepata jawabu la maana ya kifo. Kwa sababu ni bayana kuwa ni vigumu sana kutenganisha maisha na kifo. Hivyo basi binadamu anajikuta akikabiliwa na kifo na hapati njia ya kukikwepa.

Kama tulivyoona hapa, matapo yote mawili yanakubaliana kuhusu udhaifu wa maisha ya binadamu. Binadamu ambaye daima ni mdhaifu anakabiliwa na unasibu usioisha na unaomuhitaji kubadilika badilika kukabiliana na mabadiliko haya.

## *1.9 NJIA ZA UTAFITI*

Utafiti wetu umejikita katika maktaba. Tutazisoma riwaya za *Kichwamaji* na *Dunia Uwanja wa Fujo.* Vilevile tutazisoma kazi zingine zilizotangulia katika uhakiki wa riwaya hizi ambazo zinahusiana na somo letu la utafiti. Hizi ni pamoja na tasnifu, majarida na makala mbalimbali.

Hatukuwa na budi kuzipitia kazi mbalimbali za waandishi walioeleza kuhusu nadharia na falsafa ya udhanaishi kama Warnocks M., Faulquine P., Heinemann F., Roubiczek P, Greene N, na wengineo. Kazi hizi zitatufaa katika kuifahamu nadharia hii ya uhakiki wa fasihi na kuweza kuitumia ipasavyo.

Ni matumaini yetu kwamba, mawazo yao yataendelea kusukuma mbele utafiti wa fasihi. Vilevile, tumetumia tajriba yetu kama wanafasihi. Maoni na mawazo yetu yatatusaidia kuyapanua mawazo yetu katika kuikamilisha tasnifu yetu. Tutatafuta maoni kutoka kwa wasomi wenzetu pamoja na wataalamu wa fasihi.

# SURA YA PILI

## DHAMIRA NA MOTIFU ZA UDHANAISHI KATIKA RIWAYA YA KICHWAMAJI

### 2.0 UTANGULIZI

Katika sura hii ya pili, tunadhamiria kuichambua riwaya ya Kichwamaji tukionyesha dhana ya maisha tukitumia mihimili husika ya nadharia ya udhanaishi. Vilevile tumetoa mfano katika riwaya ya *Rosa Mistika* kumpa msomaji taswira kamili ya uhusika unaoelekeza uamuzi wa utumizi wa nadharia husika kukpitia kwa Rosa na kutuondolea tashwishi kuhusu dhana ya maisha.

### 2.1 UKATAJI TAMAA KATIKA RIWAYA YA KICHWAMAJI

Ukataji tamaa ni mojawapo wa mihimili ya udhanaishi. Mhusika mkuu Kazimoto anaonekana kukata tamaa na kupoteza matumaini mara kadha wa kadha katika riwaya hii. Kazimoto anaonekana kukubali na kukiri kwa kinywa chake mwenyewe kwamba amekata tamaa. Katika uk 48, tumwona Kazimoto akiwa amemtembelea Kamata rafikiye ambaye alikuwa tayari amemwoa Matilda. Anapoulizwa na Kamata masuala ya ndoa; utaoa lini? anajibu sijapata bado msichana anayenipenda. Yeyote nimwendeaye ananirusha mwishowe nimekata tamaa.

Vile vile, tunazidi kumuona Kazimoto katika hali ya kukata tamaa karibu mwishoni mwa hadithi, pale ambapo anakumbwa na janga la kifo cha mwanawe. Mke wake Sabina anabeba mimba vizuri lakini inapofika wakati wa kujifungua, mtoto anazaliwa na kuishi kwa saa moja tu kisha anaaga dunia kwa sababu alikuwa na kichwa kikubwa kupita kiasi

na mke wake alipata shida ya kuweza kupitisha kichwa cha mtoto huyu. Kazimoto anasema:

> Baada ya mazishi tulirudi nyumbani mikono mitupu. Matumaini yetu yote yalifutika kwa urahisi kama mwalimu afutavyo maandishi yake ubaoni ambayo bado hayajanakiliwa na wanafunzi. Tuliona matumaini yetu yakifutika, lakini nani aliyeyafuta? Kweli tulirudi nyumbani mikono mitupu- mimi na mke wangu. (uk 180)

Kazimoto alianza tena kufikiri juu ya Mungu, kama kweli Mungu alikuwapo hakuona kwa nini aliweza kufanya ukatili mkubwa kama huo. Alikata tamaa ya kuishi na anamwambia mke wake,

> Mimi nimekata tamaa, nilimwambia mke wangu. Tamaa ya nini? Aliniuliza kwa Sauti yenye masikitiko mengi, ya kuishi-kupata watoto. (uk 180)

Japo Sabina mke wake anamueleza kuwa yeye bado yuko na matumaini, na kwamba yale yalikuwa ni majaribu tu, wafaa wawe wavumilivu. Sabina aliyaona maisha katika ngazi ya tatu ya kidini, kama alivyoyaona maisha mwanafalsafa wa kideni Sőren Kierkegaard kwamba utupu wa maisha unaweza kuondolewa kwa mchupo wa imani kwa Mwenyezi Mungu.

Sabina alisema:

> Mimi nina matumaini bado. Mungu ni mkubwa; anafahamu kila kitu. Anatueleza kitu kikubwa na kizuri zaidi. Anatujaribu kwa mateso ili kuona utulivu wetu.

Bwana'ngu, inafaa tuvumilie. Tukubali na tupokee lo lote lile linaloporomoshwa na Mungu juu ya maisha yetu. Yeye ndiye anayefahamu mabaya na mazuri.

Lakini Kazimoto anamfisha moyo mkewe na kunena:

Mimi siwezi kuishi tena nilimwambia kwa nini

Ulimwengu si pahali pa kuishi

Unataka kuenda kuishi wapi? Ninataka kwenda kuishi mahali ambapo ninaweza kuishi bila kufikiri na bila kujua kwamba ninaishi (uk 180).

Rukia, dadake Kazimoto ni msichana aliyekuwa na bidii za mchwa katika yote aliyokuwa akifanya. Alifanya kazi kwa juhudi kuu na Kazimoto anamsifu akisema:-

Ndugu mwanamke pekee, mwema, ndugu mfanya kazi. Uzuri wake, kama nilivyosikia watu wakisema, ulikuwa uzuri wa aina ya pekee. Uzuri ambao hata kipofu aliweza kuuona. (uk 18)

Baada ya kupelekwa kwa Manase na nduguye Kazimoto ili akasomee huko mjini, tunamwona Rukia akiwa amewekwa mimba na Manase kwa kutumia nguvu, bila utashi wake. Kisha, Manase anamfukuza Rukia. Anampa tikiti kumsindikiza hadi kituo cha basi. Alipokata tamaa ya kuendelea na masomo, anamwandikia na kumtumia Kazimoto barua na kumfahamisha yaliyojiri. Alipoipokea barua hii, Kazimoto alikereka sana na akasema moyoni.

Kulikokuwa na mwanga sasa giza!

Manase ana kiburi namna gani!

Mimi mwanamume kama yeye! (uk 20)

Manase sahibuye Kazimoto waliyesoma naye tangu wakiwa wachanga pia anaonekana kutamaushwa na matukio anayokumbana nayo kimaisha. Alipohitimu masomoni, alipata kazi na kuwa mkuu wa wilaya. Alitumia vibaya madaraka aliyonayo kwa kufuja muda wa serikali. Wakati wa masaa ya kazi, jambo kubwa alilokuwa akifanya ni kuongea na warembo ofisini; wakiwemo Pili, Vumilia na Salima ambaye hatimaye alimchukuwa kama mke wake. Tunamwona akiwa mkware kwa sababu hata baada ya kuoa, aliendelea kuwa na uhusiano wa wanawake na hata virukanjia kama Pili ambaye anamwambukiza ugonjwa wa zinaa ambao unapelekea mke wake kujifungua mtoto mwenye kichwa kikubwa, ambao ndio ulikuwa ugonjwa wa Kichwamaji.

Alipomtembelea shemejiye akiandamana na mkewe, Kazimoto alistaajabia kuona kuwa mmoja kati ya watoto wawili walioingia ndani ya nyumba alikuwa na kichwa kikubwa na akauliza kwa mshangao:

> Mtoto huyu mwenye kichwa kikubwa namna hii ni wa nani? (uk 191)

Swali hili lilileta huzuni na masikitiko katika nyumba ile maanake Salima aliondoka na kuelekea chumbani huku akilia. Baada ya kumdadisi shemejiye Manase akamwambia kisa na maana ya kitendo alichofanya Salima, akajibu.

> Umetonesha kidonda kikubwa cha mji huu. (uk 191)

Manase anakiri kwa kinywa chake kuwa hili lilikuwa janga alilolileta yeye mwenyewe. Alifafanua pia kuwa, aliendelea kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Pili hata baada ya kuoana na Salima. Ufafanuzi wa Manase unasababisha kuzimia kwa Sabina mke wa

Kazimoto ambaye alitambua sababu ya mtoto aliyemzaa akiwa na kichwa kikubwa na kufariki. Hatimaye waume hawa wawili sasa walibaini kuwa wote waliingia kwa mtego mbaya na kuambukizwa ugonjwa na Pili pasi kutambua.

Hapa ndipo tunapomuona Manase akiwa amekata tamaa kwa sababu japo alipata dawa; daktari aliyemtibu alikuwa ameaga dunia juma lililopita, na kwa bahati mbaya, vidonge vilivyokuwa nyumbani kwa daktari huyu vilikuwa vimechomwa na waliokuwa wanasafisha nyumba yake ili daktari mwingine aingie. Ilitamausha kuwa alikuwa hapatikani tena daktari mwingine! Manase anasema:

> Maisha yangu yanakuwa magumu sana. Siwezi kutoka nje ya nyumba hii isipokuwa wakati wa kazi. Nilikuwa nataka kununua gari jipya lakini mke wangu amenizuia. Anasema hataki kuona gari la kuchukulia malaya nyumbani kwake. Gari lililolala hapo nje halikuharibika lenyewe. Lilichomwa na mke wangu." (uk 193).

Hivyo basi, maisha ya Manase yako katika huzuni kubwa. Japo ametibiwa ugonjwa wa zinaa, anaishi akingoja kifo. Kuishi huku hakuonekani kuwa na faida yoyote. Kupitia kwa jambo husika, Manase anakosa maana ya maisha na anajijutia vitendo vya awali akang'amua kuwa majuto ni mjukuu huja baada ya kitendo.

## 2.2 UKENGEUSHI KATIKA RIWAYA YA KICHWAMAJI

Ni kipengele muhimu katika udhanaishi. kwa mujibu wa wafuasi wa mtazamo huu, maendeleo ya kisayansi na ya kitasnia yememkengeusha binadamu kutoka kwa Mungu, jamii na kutoka kwa nafsi yake. Katika riwaya hii, tunamuona Kazimoto akiwa amekengeushwa na elimu ya kimagharibi aliyoipata. Hivyo basi, yeye anajikuta akiwa katika upweke fulani. Tunamuona Kazimoto akisoma katika chuo kikuu cha Dar-es-Salaam na alipopata likizo, ndipo anapokuja nyumbani kuungana na jamaa yake. Anapofika, anakaa kwa muda mfupi sana kisha anaenda zake kumtembelea rafiki yake Kamata. Alipofika kwa Kamata, alijitosa mzimamzima katika anasa za dunia. Alijihusisha na ulevi na vitendo vya king'ono huku familia yake (ya mzee mafuru) ikiteseka kwa mashambulizi ya usiku. Kazimoto aliamua kuondoka bila kuaga au kutoa taarifa kwa mtu yeyote pale nyumbani.

Kazimoto alijihusisha na mambo yake binafsi na yale yanayowasibu wenzake hayamhusu ndewe wala sikio hivyo basi kujikengeusha mwenyewe na jamii. Kazimoto anaeleza kuwa:

> Asubuhi kabisa nilichukua baiskeli yangu juu juu ili isipige kelele na kumwamsha Kalia ambaye alikuwa bado usingizini. nilipoitoa nje nilifunga mlango polepole. Baba, mama, Rukia sikuwasabahi. Niliondoka bila kumwambia mtu yeyote mahali nilikokuwa nakwenda. (UK 40-41)

Walipoelekea kustarehe na rafikiye Kamata, wakiwa katika hali ya kunywa pombe, Kazimoto anajihusisha katika mazungumzo na wazee. aliwauliza wazee maswali kadha,

lakini hayakujibiwa vizuri. Aidha, Kazimoto aliulizwa maswali na wazee lakini alishindwa kuyajibu kikamilifu. Wazee pia hawakuridhika. Kazimoto anakiri kuwa alijiona yuko nje ya mazungumzo yao. Juhudi zake kabambe za kuwauliza maswali na kupata majibu ambayo hayakumridhisha zilimsukuma zaidi katika ukengeushi. Mambo yalienda mrama pale ambapo aliwaambia wazee kwamba hakuna Mungu. Wazee wote walikereka na hata ikamlazimu mmoja wao aende zake nyumbani.

> Mnazungumza na mwehu A! Anasema kwamba hakuna Mungu. Hakuna Mungu! Mtoto wa nani? mababu na mababu wamekwenda; wamechukuliwa na nani? Bangi! (uk 51)

Tunaona kwamba, hata miongoni mwa vijana waliokuwa wakilewa pamoja alikubaliana na kauli ya mzee aliyeondoka kikaoni na kuona kuwa pengine Kazimoto pombe ilikuwa imemzidi. Kijana huyu rika la Kazimoto alikuwa haoni ni kawaida mtu mwenye akili timamu kuwa na mambo aliyonena Kazimoto akasema:

> Mgeni wako ameanza kupatwa na pombe. Lakini mwambie azungumze juu ya mambo mengine au aache kabisa la sivyo ataharibu kikao. Hili linatokea kwa sababu vijana hawa hawajapata elimu aliyopata Kazimoto. Iliwabidi Kazimoto na Kamata kuhamishwa hadi nyuma ya nyumba. Kamata alijaribu kukaribisha vijana wawili zaidi waje wanywe pombe pamoja nao lakini yule alikataaa na kuwafukuza. Kazimoto aliona kwamba, mambo mengi ya dini hayana uthabiti na hivyo mtazamo huu wa kisomi ulichangia sana kumkengeusha na jamii yake. (uk 52)

Tamko hili la Kazimoto ni sawa na lile la mwanafalsafa wa Kijerumani aliyejulikana kama Friedrich Nietzsche aliyetamka "Mungu amekufa". Kulingana na hali ya matukio ilivyokuwa, Kazimoto aliafikia kwamba kizazi chake cha vijana ndicho kilichojikengeusha na wazee. Alishuhudia Salima mkewe Manase akimkaripia Mzee rika la baba yake ambaye alikuwa mfanyikazi wao wa nyumbani. Mzee huyu kachelewa kuja kazini kwa minajili ya mke wake ambaye alikuwa ameugua ghafla na ikampasa amempeleke hospitalini. anapojieleza, huku akiomba msamaha, Salima anamfokea.

> Hadithi ya mke wako, haituhusu sisi, unapaswa kufika hapa saa kumi na moja. umechelewa karibu saa mzima. Utakatwa mshahara kwanza mwezi huu umevunja karibu glasi tatu, hizo pia zitakatwa." Shauri ya kuchelewa kwako leo umetutia aibu mbele ya wageni. Tutakula saa ngapi- ebu niambie, tutakula saa ngapi? (uk 120).

Hisia za kazimoto ni kuwa wazee pengine waliwaongopa vijana kwa sababu ya elimu yao na *kwamba hawakuwa na chochote cha kutegemewa isipokuwa kufanyishwa kazi duni na* kushushwa hadhi. Vilevile hulka ya kuwakaripia watawaliwa na kuwafanya watumwa wao kama vile wabeberu walivyowafanya Waafrika katika enzi za wakoloni ni dalili za athari ya Elimu ya Kimagharibi.

Ukengeushi vilevile unaibuka pale ambapo Manase, akiwa mkuu wa wilaya anamfukuza mzee aliyekuwa ameingia ofisini mwake akiwa na fimbo. Kazimoto anaeleza kuwa, alipomsukuma mzee nje, Manase alirudi ndani kama popo aogopaye jua. Sauti ya Manase aliyekuwa sasa ananguruma kama simba iliweza kusikika. Mngurumo huu ulidhihirisha

nguvu, uwezo na mamlaka aliyokuwa nayo Manase kama mkuu wa wilaya uliompa idhini ya kumkaripia mzee, jambo lililosababisha ukengeushi baina ya watu hawa wawili. Manase alisikika akisema:

> Wazee wengine hawana akili hata kidogo! Anaingia humu na fimbo! Anafikiri humu kuna vita! (uk 2-3)

Kazimoto alihuzunika sana kuona haya na moyo wake ulivurugika kwa mchanganyiko wa hasira na huzuni alipoona mzee akikimbia serikali yake. Yeye hakuona kitu kingine isipokuwa kwamba wazee walikuwa wakikimbia vijana. Ilikuwa bayana kuwa uhusiano kati ya wazee na vijana ulikuwa umekatika, na kuleta utengano kati ya wazazi na watoto wao ambao sasa walikuwa kama simba. Kazimoto aliona wazi kuwa sasa wazee walikuwa wakiwapa vijana migongo.

Athari ya elimu ya kimagharibi haijibagui pale ambapo Manase na Kazimoto wanajadiliana kuhusu muziki wa Kizungu. Manase anazilinganisha na kusema;

> Hivi muziki wa Kiafrika unakupendeza nini? Unalia mbu! Mbu! Mbu! Tangu mwanzo mpaka mwisho. Mwishowe unaleta mbu ndani ya nyumba….. Hauna ile hali ya kupanda juu na kushuka chini kwa sauti ambazo zimekadiriwa na kupimwa kwa ufundi na usanifu wa mziki ili kuleta wazo fulani la undani linalokuja polepole na kungia moyoni kwa utulivu na kusambaa katika damu mwili mzima. Muziki wa Kizungu wa mapenzi ukilia unaweza kuona picha ya watu wakipendana au picha ya mwimbaji mwenyewe. Unafurahisha moyo na

mwili mzima hata wewe msikilizaji unajiona kwamba hukanyagi chini. Yaani umekuwa kama unachukuliwa na mawingu........ (uk.118 )

Matamshi haya ya Manase yanaonyesha vile anavyochukia utamaduni wake na kuegemea utamaduni wa Kizungu. Hivyo basi, vijana wamejikengeusha na utamaduni wao. Vijana wanataraji kazi za hadhi, mishahara mikubwa huku wakijirusha na kuabudu ule wa kigeni walioupata katika usomi wao. Wanakengeuka na utamaduni wa jamii zao.

Katika riwaya hii, ukengeushi vilevile unaonekana pale ambapo Rukia dadaye Kazimoto anajitenga na mazingira yake kufikia kukosa tamaa ya kula kwa uchungu moyoni na hasira alizokuwa nazo baada ya kutungwa mimba na Manase kwa nguvu ilihali yeye alikuwa na ari sana ya masomo. Wakati wa kujifungua, Rukia anakosa nguvu na kuaga dunia. Tuza, mkewe Kabenga jirani yao, anamweleza Kazimoto:

> Ndugu yako amekufa kwa sababu amekosa nguvu; alikuwa hajala vizuri kwa muda mrefu uliopita. (uk 83).

Kifo cha Rukia kinasababisha kifo cha mamaye ambaye analalama kuumwa na kichwa, kutotoma na kuanguka chini na kufa papo hapo kwa ajili ya masikitiko ya kumpoteza mwanawe. Vifo hivi vinaletwa na ukengeushi uliopo katika riwaya ya *Kichwamaji.* Rukia amekengeushwa na nduguye Kazimoto na jamii yake kwa ujumla naye mamaye amekengeushwa na maisha yenyewe.

Katika Riwaya ya *Rosa Mistika,* tunamwona Rosa ambaye alilelewa na babake mzee Zakaria kwa ukali mkuu anaamua kuishi maisha tofauti anapojiunga na shule ya upili

nyakati hizo. Kabla ya kujiunga na shule hiyo, hakuwa anamjuwa mwanamume. Katika shule hii ya upili, sasa anaonekana kuanza mkondo mpya wa maisha na hapo awali.

> Rosa sasa alianza mapenzi. Alianza mapenzi lakini aliyaendea haraka sana kama mbwa aliyekata kamba. Aliona mvulana mmoja au wawili walikuwa hawamtoshi kwa urafiki. Mwaka huo huo aliwakubalia wavulana watano............. (uk.33)

Alipokuwa sasa amekuwa mkufunzi katika jambo hili na kujitosa mzimamzima katika starehe na anasa za dunia, alikumbana na changamoto kadhaa. Anakata shauri kujiua na hivyo kujikengeusha na kutengana na nafsi yake. Hata pale ambapo padri anakuja kumhubiria, yeye anakataa katakata na kuonyesha kutokuwa na haja katika mahubiri hayo.

Katika kulitazama suala hili la ukengeushi tunagundua kuwa, kunao ukengeushi baina ya wasomi wenyewe; yaani wale hasa walioathiriwa na utamaduni wa Kizungu na kuutupilia mbali utamaduni wao wa Kiafrika. Baina ya wasomi kuna viwango tofauti. Kuna wale waliofaulu kimaisha (kiuchumi) kimamlaka, na wana uwezo zaidi ya wengine. Tunamuona Kazimoto akinyimwa kazi na Manase ambayo inaonekana ilikuwepo lakini kwa vile alikuwa ametunukiwa madaraka yale, alikataa kumuajiri bila sababu ya kuridhisha japo alikuwa tayari ni mwanafunzi katika chuo kikuu na walikuwa wanajuwana. Kwa hivyo, iwapo kuna watu/mtu au tabaka lenye nguvu na uwezo, msomi, hata aliyehitimu inambidi anyenyekee huku akikabiliana na unyanyasaji wa hali ya juu kutoka kwa msomi mwenzake. Kwa ujumla, tunabainisha hapa kuwa binadamu amekengeushwa na Mungu, jamaa au familia yake na nafsi yake mwenyewe.

## 2.3 SUALA LA UTEUZI KATIKA RIWAYA YA KICHWAMAJI

Uteuzi ni mojawapo wa mihimili ya udhanaishi. Hapa mwanadamu anapaswa kufanya uteuzi; si swala la hiari, ni lazima afanye huo uteuzi. Vilevile, katika uteuzi anaofanya binadamu, anatakiwa awajibikie matokeo na athari za uteuzi wake. Uwe mbaya au mzuri. Maisha ya kujizamisha kwenya anasa za dunia kama vile ulevi na kujihusisha na vitendo vya ngono ndio chanzo cha mikasa na maafa yaliyompata Kazimoto. Tunamwona akijihusisha na uhusiano wa kimapenzi na wanawake wengi wakiwemo vumilia, pili, nyabuso na Sabina ambaye hatimaye alimuoa. Mazungumzo kati yake na Manase, Shemejiye yanafichuwa siri juu ya ugonjwa ambao alimwambukiza mkewe Sabina hata ndipo kitoto chao kikazaliwa na kichwa kikubwa kilichopelekea kufa kwake saa moja tu baada ya kuzaliwa. Mashemeji hawa walifanya ngono na pili aliyewaambukiza ugonjwa huu hatari.Isitoshe Kazimoto aliendelea kuwa na uhusiano huu hata baada ya kufunga ndoa na Sabina.

Mtoto wa Manase kadhalika alikuwa amezaliwa na kichwa kikubwa na aliwashangaza wote waliomuona japo Kazimoto hakubainisha kwa mkewe Sabina kuwa alikuwa na uhusiano na pili, barua ya masikitiko aliyopewa Helena aliyekuwa mpishi wao na pili ni dhihirisho kuwa uhusiano wao ulikuwa haujakoma. Pili naye alikwisha elewa kuwa kamwambukiza Kazimoto. Ugonjwa huu ndio unaomfanya Kazimoto autowe uhai wake hatimaye, hivyo basi akawa uteuzi aliofanya ameuajibikia. (uk 191 – 192).

Kazimoto anahiari kumkata Manase vipande vipande ili kulipiza kisasi cha Manase kumharibu kwa kumtia mimba dadaye (Uk 13). Kazimoto anakabiliana na tatizo la

kutaka kumchoma Manase visu vy tumboni, lakini anachelea kwa sababu dhamiri yake inamwambia kwamba akifanya hivyo huenda akanyongwa na basi akaogopa.

> Wazo la kufika tu ofisini nimchome Manase visu vya tumboni lilinijia, tena kichwani huenda nami nikanyongwa (uk 15).

Kazimoto anateua kulipiza kisasi kwa kutaka kumtia mimba Sabina kisha amuache kama vile Manase alivyomfanyia Rukia lakini anaishia kumuoa Sabina na kuwa mashemeji na Manase.

Vilevile tunamuona kazimoto akiwa amefanya uteuzi wa kumtumia Kalia nduguye kama posta. Daima aliandamana na Kalia katika safari zake za kumchukuwa Vumilia nyumbani kwao. Tabia hii ilimfanya Kalia kuiga tabia husika. Yeye alichipuza kuwa hatari zaidi maanake tunamuona baadaye anatembea na Tegemea, mamake vumilia na mara kwa mara alilala huko. Kalia alizidi kuwa gwiji kwa sababu alianza kuwashika kwa nguvu wanawake na wasichana wa shule. Jambo hili lilimfanya akaitwa nunda mla watu. Hata babake Kalia alimfukuza akisema:

> Sitaki kukuona tena mjini kwangu. Na hata nikifa usije kula mbele ya kaburi langu (uk 111).

Kalia alifukuzwa kijijini lakini kwa utundu wake hakuondoka. Vitendo hivi hatimaye vilisababisha kifo chake. Alipatikana mtoni akiwa amechomwa mikuki ya tumboni na kifuani (uk 14).

Kifo cha Kalia kilimsumbua moyoni Kazimoto kwa sababu aliona kuhusika nacho.

> Kifo chake kilihusika Sana na matendo yangu. Ilikuwa kama kwamba

> mimi mwenyewe nilimuua mdogo wangu. (Uk 195)

Kazimoto vilevile anakiri kuhusika na kifo cha Kalia ingawa hakumgusa.

> Mimi, kabla ya kufa, ninaungama mbele ya ulimwengu kwamba nilimwua mdogo wangu ingawa sikumgusa. (uk 195).

Uteuzi aliofanya Kalia wa kuiga tabia ya Kazimoto na hata kuibuka mahiri zaidi ya kakake, uliosababisha kifo chake, ulihuzunisha kila mtu. Uhusiano baina yake na Tegemea mamake Vumilia ulikuwa ni fedheha tosha katika familia yake. Habari za kifo chake zinapoletwa na mzee Kabenga, Babake alinyamaza kwa muda mfupi halafu alifungua kinywa chake akanena:

> Mababu na mababu walizoea kuoga katika mto huu ili kuondoa uchafu wa mwili wao. Wafiwa walifua humo nguo zao ili kuondoa maafa yote ya kifo; maprotestanti walipokuja waliutumia kuondoa dhambi za roho. Watoto wetu sasa wamekuja wameuchafua kwa kuozea humo ndani. Kitu gani kitawaosha sasa na kuwatakasa? Kweli mimi nimelaaniwa kuona kwamba jambo hili limetokea nyumbani kwangu nami bado nikiishi!

Hii inamaanisha kuwa mzee huyu anaona ni heri Mungu angekuwa amemchukua mapema asiyaone aliyokuwa anayaona sasa. Isitoshe, babake kalia alikataa kuita polisi. Tunaelezwa pia kuwa, kila mtu kijijini alifikiria kifo kilichompata kilikuwa cha haki na kwamba angeishi angeleta maafa mengi zaidi. Vilevile kijiji chote kilifahamu lakini wachache walihudhuria mazishi.

## 2.4 DHAMIRA YA KIFO KATIKA RIWAYA YA KICHWAMAJI

Mhimili huu unadhihirika kulingana na maafa yaliyompata Kazimoto aila yake pamoja na ile ya babake. kulingana na wanaudhanaishi, juhudi zote za mwanadamu za kuboresha maisha zinaambulia patupu manake zinazimwa na kifo. Juhudi zake za kujitafutia maana ya maisha mara nyingi huishia katika mvunjo au uvunjikaji wa juhudi hizo, hasa katika mauti. Mwisho wa mwanadamu ni kifo. Jumla ya vifo vitano vilivyomkumba Kazimoto ni dhihirisho kuwa, kifo chamuandama mwanadamu wakati wowote, mahali popote maishani mwake. Vifo hivi ni kifo cha Rukia dadaye Kazimoto, kifo cha mamaye kazimoto, kifo cha Kalia nduguye Kazimoto, kifo cha mwanawe na hatimaye kifo cha Kazimoto mwenyewe.

Anavyowazia mwandishi wa riwaya hii kuhusu suala la kifo ni sawa na wanafalsafa Karl Peters, Jean Paul Satre na Martin Heidegger. Vifo hivi vimemwacha Kazimoto na fikra nyingi. Kwanza kilianza kifo cha Rukia ambaye alifariki wakati alijifungua kwa ajili ya kukosa nguvu. Baada ya kifo cha dadake, Kazimoto aliingia katika kilindi cha mawazo juu ya kifo chake mwenyewe.

> Usiku nilianza kufikiria juu ya kifo; nilifikiria jinsi kifo changu kitakavyonijia kwa ugonjwa, kwa ajali au kwa kukatwakatwa na wezi? Labda kwa uzee au kwa sumu! Huenda nikajiua mwenyewe (uk. 84).

Hapa tunamwona Kazimoto akiwa anatabiri kifo chake mwenyewe kwa sababu hadithi inapotamatika anajipiga risasi na kuufunga ukurasa wa maisha yake yaliyokumbwa na changamoto tele. Baada ya kifo cha Rukia, kilifuata kifo cha mamaye ambaye wakati

msichanawe alipoaga dunia, alilalamika kuumwa na kichwa, kuanguka, kuzimia na hatimaye naye akaipa dunia kisogo.

> Rukia! Rukia! "Hali akionyesha kwa mkono wake kaburi. Halafu anaanza kulia kwa namna ya pekee," kichwa, Kichwa! alitotoma na kuanguka chini. (Uk 85).

Muda si muda kilifuata kifo cha nduguye mdogo Kalia ambaye alipatikana mtoni akiwa ameuawa kwa kudungwa mikuki miwili, mmoja tumboni, mwingine kifuani kufuatia vitendo vyake viovu vya kuwabaka wasichana na wamama. Kifo cha Kalia ndio labda kinamfanya Kazimoto aseme kuwa kifo anachoogopa zaidi ni cha majini.

> Mna habari? Kabenga alianza kusema "Mwili wa Kalia umekuwa ukielea majini huko mtoni kwa siku mbili. Watu wameuona, lakini hakuna mtu apendaye kujiweka hatarini. Mwishowe nimejitolea kuja kuwaambia. Heri tukautoe kabla haujaharibu maji yote ya mtoni, watu wakakosa mahali pa kuoga?. (uk 114).

Kama kutonesha kidonda, masaibu yaliendelea kumwandama Kazimoto pale ambapo mkewe Sabina anapojifungua mtoto mwenye kichwa kikubwa kupita kiasi na kuenda jongomeo baada ya saa moja.

> Mke wako alipata shida ya kuweza kupitisha kichwa cha mtoto ambacho kilikuwa kikubwa kupita kiasi. Daktari alichelewa kufika. Alipokuja mtoto alizaliwa lakini aliishi kwa muda wa saa moja tu. Tulifanya tulivyoweza ili kuokoa maisha yake, lakini kwa kuwa hakuzaliwa ili apata kuishi, alirudi. (uk 179).

Mwandishi anapotamatisha riwaya hii, tunamwona Kazimoto anakata shauri kujiua kwa kujipiga risasi. Hii ni kwa sababu baada ya kuzungumza na Manase, anagundua kuwa alikuwa ameugua ugonjwa usio na tiba na hivyo alijihesabu kama mfu.

> Nimejiua, siwezi kuendelea kuzaa kizazi kibaya. Pia sikuona tofauti kati yangu na mdudu au mnyama. Mtu yeyote asilaumiwe kwa kifo changu. (Uk 195)

Tumeona motifu ya kifo kikiwa kimetawala riwaya nzima. Vifo vilivyosababisha maasi mbalimbali vinaonekana na kila kitendo kinatokea kiusababishi, kila kifo kimesababishwa na jambo fulani. Hata hivyo katikati ya riwaya hii, tunamuona Kazimoto akiwa anaitafsiri ndoto ya Kalia kutizama kifo kwa muelekeo tofauti kabisa. Kazimoto aling'amua kuwa kifo ni kugeuka hali. Ilikuwa bayana kuwa waliokufa bado wangalipo, lakini katika hali tofauti, Kazimoto asema:

> Kwanza kufa ni kugeuka hali – yes, a change of state," nilisema kwa Kiingereza. (uk 75)

Mwanafalsafa Gabriel Marcel alikuwa na maoni kama haya. Marcel alikiri kuwa, kifo ni mwanzo tu wa maisha ya milele. Wanaounga mkono jambo hili basi watakuwa na imani kuwa watu hawa watano wa aila ya Kazimoto ndio sasa walikuwa wameanza safari ndefu ya maisha ya milele.

## 2.5 HOFU, KIHORO, DUKUDUKU KATIKA RIWAYA YA KICHWAMAJI

Maisha ya binadamu yanadhibitiwa na (hofu, kihoro na wasiwasi). Jambo hili humfanya binadamu akose kujuwa la kufanya. Jambo hili linafanya maisha ya binadamu yasiwe imara wala kuwa na msimamo unaofaa. Alipopata likizo pale chuo kikuu, Kazimoto alihiari kuja nyumbani ili kupumzika na kuwanga kichwa chake kwa ajili ya masomo. Alipofika kwao, alipata vituko vilivyomfanya hata ajutie kufika kwake. Ilikuwa kwamba watu hawana utulivu na hawalali kwa sababu kuna waovu fulani ambao humwaga mchanga nyumbani mwao inapofika usiku.

> Siku nzima sikuwa na raha. Nilikuwa nafikiria jambo la kufanya. Hata chakula cha mchana sikula vizuri. Baada ya kula nilijaribu kusoma hadithi lakini niliona kwamba nilikuwa sifuati. (uk 31)

Vile vile, tunamuona kazimoto akikiri kuwa, baada ya kifo cha mtoto wake, alibaki katika hofu na huzuni kubwa.

> Sisi tuliendelea kuishi, tukawa tunasukumwa mbele na huzuni. Upepo wa maisha. (uk. 181)

Tamko hili ni sawa na lile la mwanaudhanaishi wa imani Martin Heidegger aliyeamini kuwa binadamu ni mnyonge na hana hiari na matukio ambayo anashuhudia maishani mwake. Kulingana na Heidegger matukio haya hutokea kama ajali maishani mwake.

## 2.6 MSAKO WA MAANA YA MAISHA KATIKA RIWAYA YA KICHWAMAJI

Kwa mujibu wa nadharia na falsafa ya udhanaishi, binadamu huishi akijiuliza maisha ya mwanadamu yana maana gani? au yana haja gani? Kuweko kwa mwanadamu kuna umuhimu gani? Kuna maana gani au lengo gani katika matendo ya mwanadamu? Mwanafalsafa Sőren Kierkegaard aliweza kujiuliza maswali haya. Kierkegaard alimwona binadamu kama kiumbe anayeteseka na anayeishi katika ulimwengu usiomjali, aliyezungukwa na mateso na ubwege na anayeshindwa kukabiliana au kupatana vyema na uhalisi huo. Kazimoto anasumumbuliwa na mawazo kama haya kufuatia na baada ya kifo cha dadake Rukia. Yeye alionelea kwamba, jambo linalomsumbua binadamu ni maisha yenyewe. Anahisi kwamba, adhabu kubwa kwa binadamu ni maisha yenyewe. Kazimoto anasema:

> Niliona kwamba adhabu kubwa ya mwanadamu ni maisha yenyewe. (Uk 84)

Kazimoto alikumbuka mlevi mmoja aliyemkuta akipiga mti mweleka mpaka akaumia mwenyewe. Anaona kuwa, maisha ndiyo yaliyokuwa yakimsumbua wala si pombe. Vilevile alishangaa ni kwa nini mwanadamu alijidai kupiga mpira kwa kichwa kitunzacho bongo. Kazimoto anasisitiza akieleza kuwa yote mwanadamu mwenye akili anafanya kuwa jina ambalo limempumbaza akili. Jina 'Furaha' ambalo ni neno jingine la adhabu.

Kazimoto anabainisha kwamba hii ni adhabu ambayo kila mwanadamu amepewa kutunza maisha yake. Maisha ambayo hayashibwi wala kuridhishwa. Zaidi ya hayo, mwenye nguvu anatunyang'anya maisha haya wakati wowote bila hata kutuarifu. Hii

inamaanisha kwamba, mwanadamu hana budi kusalimu amri mbele za Mungu. Mungu ndiye mwenye uweza wa yote na punde tu anapoamua kuyakatiza maisha ya mja, basi jambo hili halipingiki.

Kazimoto anatoa mfano wa adhabu ya yule mtu aliyeamrishwa kujaza maji ndani ya pakacha. Kwamba, sisi wanadamu tumekubali kufanya hivi kwa jina la "Furaha" maisha matamu! Yaani adhabu ni tamu. Kazimoto anaonelea kuwa mwanadamu hana akili kwa sababu kama angekuwa na akili angekataa adhabu hii, ni kama yule ambaye ametupa adhabu hii angetushurutisha tungejua sote.

Mwanadamu ni kiumbe ambaye amejaribu kutafuta njia nyingi zitakazomwezesha kupata furaha kwa kuwa ameshindwa kupata furaha hapa duniani amejenga kichwani mwake kifo kama pingu, yaani mahali anapotegemea kupata furaha baada ya kufa. Ibara hii inamaanisha kwamba ni vigumu kupata furaha hapa duniani. Dini imeletwa na mwanadamu baada ya kuona kuwa ameshindwa kupata furaha hapa duniani.

Albert Camus ndiye mwasisi wa kiudhanaishi ambaye alishughulikia suala la furaha katika maisha ya mwanadamu. Camus anaeleza kuwa, hakuna furaha katika maisha ya binadamu na kwamba kila furaha ina kinyume chake. Kupitia kwa Kazimoto, Kezilahabi anatoa mfano wa maji yateremkayo kuelekea ziwani. Kazimoto anaeleza:

> Nilianza kufikiri kama kweli maisha ya binadamu yalikuwa hayawezi kulinganishwa na maji yateremkayo kutoka mlimani kwenda ziwani au baharini. Maji haya yalikuwa yakiteremka kwa kasi sana; kurudi juu yalikuwa hayawezi.

> Yalikuwa hayasukumwi na nguvu kutoka nje isipokuwa yalikuwa yakienda tu kwa sababu kulikuwa na mteremko. Yatake yasitake yalipaswa yateremke. (uk 90).

Dondoo hii inamaanisha kuwa katika kuishi kwake, mwanadamu hana budi kufa na hata akijaribu mbinu zipi, hataweza kufanikiwa. Mwisho wake ambao unaonekana kupangwa na mwenye nguvu, mwenye enzi na dunia, sharti uhitimike bila kubahatisha. Anapopambana na safari yake ya maisha, kama vile mto ukusanyavyo taka, mwanadamu hukusanya taka nyingi kitambo afikie kikomo cha maisha yake Kadiri ya muda alioishi. Kazimoto anaona heri angekufa angali mtoto kuliko kukumbana na masaibu haya.

Mwandishi vilevile ameangazia suala la furaha katika maisha ya unyumba. Analinganisha maisha katika ndoa za wasomi Kazimoto na Manase na ndoa ya Kamata. Alipooa, Kazimoto anaishi maisha ya furaha sana na mke wake Sabina hata tunamwona pale ambapo wanapoteza muda mwingi muhimu wakitafuta majina ya kuitana, mpaka pale ambapo wanaafikiana.

> Kila siku Sabina," alifoka, "wengine wanaita wake zao Maggy, Betty, wewe kila siku Sabinaa! Sabinaa! Unataka Kusabina nini? Mapenzi gani hayo! (Uk 157).

Wakati huu, penzi lilikuwa limenoga vilivyo, lakini baadaye tunaona ndoa hii ikiwa imezama katika zogo kuu baada ya siri kufichuka katika ziara ya Kazimoto na mkewe walipotembelea shemejiye Manase. Sabina azimia katika mazungumzo haya na huo ukawa mwanzo wa matatizo ulioishia katika kifo cha Kazimoto.

Manase hali kadhalika wanakuwa na ndoa ya furaha mwanzoni, gari nzuri, mkuu wa wilaya na mkewe Salima akiwa mwalimu. Baadaye, inasikitisha tunapoona furaha hii ikipotea kwa sababu ya ugojwa wa zinaa uliowaingia. Kwanza, wanapata mtoto mwenye kichwa kikubwa kupita kiasi, na pili tunaona afya ya Salima ikiwa imedhoofika na wanaishi kwa madawa. Kando na kutowajibika nyumbani kwa mambo kama usafi, Salima analichoma gari lao kwa hasira za kwamba linatumika kubebea viruka njia walioleta kilio cha milele katika aila ile.

Ndoa ya Kamata na Matilda ambao walikuwa na elimu duni, ilikuwa yenye furaha tele. Dosari tu, ni pale ambapo Kamata anapigwa na watu ambao wanamtamani mke wake. Mwandishi anatoa wazo kuwa japo kuna furaha katika maisha ya mwanadamu, furaha hii hudumu kwa nadra sana.

Siku ile Kazimoto na mkewe waliwatembelea Manase; kunaibuka mifano kadha inayotuonyesha ukosefu wa maana ya maisha ya mwanadamu. Kwanza, kuna sanamu ya kimakonde inayoeleza taabu za mwanadamu hapa duniani. Sanamu hii inatufunulia kuwa, hata mwanadamu afanye nini, mwisho wake ni kaburini. Hii inamaanisha kuwa, juhudi zake zote akiwa duniani zitaambulia patupu pale ambapo mwenye nguvu, yaani Mungu anapoamua kumhamisha ulimwengu wa pili. Mwanaudhanaishi Albert Camus alidai kwamba furaha ya kudumu haiwezi kupatikana katika maisha ya binadamu. Manase alieleza;

> Ukitazama sanamu hii vizuri, aliendelea, "Utaona mambo mengi." Aliinuka. Alishika sanamu hiyo mikononi mwake.

Kwanza utaona kwamba inatueleza taabu za binadamu hapa duniani. (uk. 185) Pia inaonyesha jinsi kifo kinavyomjia mwanadamu. Ukiitazama kwa makini, unaweza kuona kichwani mwako picha ya mtu amelala kaburini, meno nje akicheka sisimizi. Utaweza kupata lile wazo kwamba sisi wanadamu hatuna chochote cha kujivunia". Ukweli ni kwamba sisi wanadamu tunakufa polepole; kaburini hatua yetu ya mwisho tu. (Uk 185-186).

Kulingana na dondoo hii na maoni ya mwandishi, mtu anapokuwa akiendelea kuishi, anaendelea kufa (kifo cha polepole) hadi atakapofikishwa kaburini ndicho kifo halisi. Manase anamtia woga Kazimoto anapomfahamisha kuwa siha yake ilikuwa imebadilika, alikuwa amekonda sana, naye bila pingamizi anatambuwa ukweli huu na kukiri. Manase anamwambia:

> Mabadiliko hayo ndiyo yanakufanya uwe unakufa polepole; kaburi ni hatua ya mwisho tu ya tendo lilelile. (Uk 186)

Maelezo ya mafungu haya yanawiana na yale ya Samuel Beckett, mmoja wa waandishi wa awali ambaye alikuwa mwanafalsafa mashuhuri wa udhanaishi. Yeye, sawasawa na Kezilahabi anaamini kuwa, mtu anapoishi huwa anakufa polepole na hatimaye hufa kabisa. Kulingana naye, maisha ni kuendelea kufa, hadi pale ambapo kifo cha kweli kinapotukia.

Kisha Manase anamwonyesha Kazimoto ngozi ya simba aliyekuwa ameua watu kumi kwa muda wa siku tatu. Anaeleza kuwa, madhumuni ya kuweka ngozi ile ni kumfanya

kila mtu aingiaye ndani ya nyumba hii aogope. Manase anafafanua kuwa, mtu yeyote aonaye ngozi ile atafikiri juu ya maisha yake lakini kwa kuwa haoini kitu tena kwa sababu ya wuoga, polepole ataanza kuona kwamba maisha yake hayana maana. Mnyama kama yule angeweza kupokonya wanadamu maisha yao kwa urahisi sana. Alihitimisha maelezo haya kwa ufasaha mkubwa kwa kumfahamisha shemejiye kuwa wenyeji wa mastakimu yale, yeye na mkewe walikuwa hawaoni tena maana ya maisha. Jambo hili lililenga mawazo na maoni ya Kazimoto kuwa hata yeye alikuwa mwadhiriwa wa hali hii.

Msisitizo unafanywa na Manase pale ambapo anamfananisha mwanadamu na samaki mtegoni. Samaki huyu anajikazatiti kadiri ya uwezo wake kujinasua bila mafanikio. Hili asema Manase linaonyesha kwamba matatizo ya binadamu ni magumu na hayawezi kutafutwa jawabu kwa urahisi.

> Mwanadamu kama samaki, atajaribu kujikakamua lakini kazi bure (Uk 188).

Mwandishi anatuchorea ramani iliyo wazi kabisa kuwa, licha ya kuwa maisha yanaonekana kutokuwa na maana, yanaonekana kupangwa kabisa Hii ni kumaanisha kuwa, katu mwanadamu hawezi kubadilisha maisha yake; la hiari hana, kwa sababu safari yake yote tangu kuzaliwa hadi mwisho imepangwa; lake ni kukubali yaishe.

Ithibati iliyo wazi kuhusu kwamba maisha ya mwanadamu yamepangwa kabisa ni maisha ya Kazimoto mwenyewe. Pale mwanzo ambapo Manase amemtunga mimba Rukia na

kumharibia masomo yake, anahiari kuchoma nyumba ya akina Manase; jambo lililoleta kuumia, kuchomeka mkono kwa mamake Manase, Tuza ambaye baadaye anakuwa mkwewe baada ya kumuoa sabina kwa nia ya kumtia mimba na kumuacha ili kulipiza kisasi. Ni baada ya kumuoa Sabina ambapo wanapata mtoto mwenye kichwa kikubwa kupita kiasi na kuzaliwa kwa mtoto huyu; chanzo cha kichwa hicho kinajulikana wakati Kazimoto wanamtembelea Manase. Hali hii ndiyo iliyosababisha Kazimoto akaamua kuchukuwa bastola na kujipiga risasi.

Kupitia kwa wahusika hawa wawili, Kazimoto na Manase, Kezilahabi anatupa suluhisho la kupambana na maisha haya ya kufisha moyo. Kazimoto anahiari kujuwa ati asiendelee kuzaa kizazi kibaya. Aliona achukuwe njia ya mkato. Hata hivyo, ni vyema kufahamu kuwa, kujiuwa si suluhisho halisi, kwa sababu huku ni kukwepa ukweli wa maisha. Tunatakiwa kujitolea kukabiliana na ugumu wa maisha pamoja na shinikizo zake.
Manase naye anaamua kuishi akingoja kifo chake. Tayari walikuwa wameshatambua kuwa mtoto waliyemzaa kadhalika ana ugonjwa huohuo. Japo anajikaza kiume kuyaishi maisha haya; anaishi kwa simanzi na fedheha tele na ni mkosefu wa matumaini. Mwanaudhanaishi Albert Camus kutoka Algeria alifahamika kutoa suluhisho hizi zote mbili ambazo Kezilahabi amezitoa hapa.

## 2.7 SUALA LA MUNGU KATIKA RIWAYA YA KICHWAMAJI

Udhanaishi ni falsafa inayozungumzia uhusiano uliopo kati ya mtu na Mungu, na iwapo mtu anapaswa kuamini kuwepo kwa Mungu. Mawazo ya Kezilahabi kuhusu Mungu yanaoana na yale ya Martin Heidegger na Karl Jaspers. Waasisi hawa wanaamini kuwa, wale ambao wanaamini kuhusu kuwepo kwa Mungu na wamejitosa katika dini ni mbinu ya kujificha kutokana na woga unaowakabili katika maisha ya kila siku.

> Woga umeleta Mungu, anajiwazia Kazimoto, na woga umeletwa na mambo yote yanayomzunguka mwanadamu. Na ujasiri je unaleta nini? Nafikiri utaleta kutoamini Mungu. (Uk 125 ).

Kulingana na wanafalsafa hawa, kwao kwamba Mungu yuko au aliumba ulimwengu ni suala ambalo hawalishughulikii kwa sababu halioani na mantiki ya fikira zao. Kwa mujibu wa mwanaudhanaishi Sőren Kierkeggard, inakuwa vigumu kuyakinisha kuwako au kutokuwako kwa Mungu; kwa kuwa maarifa aliyonayo binadamu yana kikomo. Mwanaudhanaishi Paul Tillich, anatoa maoni kuwa binadamu hujaribu kuelewa dunia, lakini anakumbana na matatizo pacha yasiyokuwa na kikomo. Hivyo basi kuishia kuwa na imani kwa Mungu ili kuziba lile pengo linalotokana na ukosefu wa maelezo.

Wamitila K.W. (2003: 248) anaeleza kuwa, Kierkegaard katika maandishi yake *"The Concept of Dread, Fear of Trembling* na *Sickness unto Death,"* anakiri kuwa mwanadamu hupata kimbilio kutoka mivutano ya maisha kupitia kwa Mungu. Hii ni imani ambayo iliishia kushika nguvu sana katika Ukristo.

Mwasisi Pascal Blaise naye alidadisi, "tunawezaje kuamua ikiwa Mungu anaishi au haishi? Hili ni fumbo la mwanadamu. Swala la utata hapa ni kule kuwepo au kutokuwepo kwa Mungu. Katika Riwaya hii, tukio la kushangaza linatokea pale ambapo Salima analeta chakula mezani. Ni Sabina na Salima ambao waliomba dua kabla ya kula chakula, Kazimoto na Manase hawakuomba na walitazamana kwa mshangao lakini wanajiunga kushambulia chakula pindi tu maombi yalipohitimishwa.

Kazimoto alinena, mimi na Manase tulitazamana kama kwamba tulikuwa tukiulizana "wanafanya nini". Walipomaliza kuomba dua, tulianza kushambulia. (uk 189)

Suala la Mungu linajadiliwa kwa kirefu na Manase na Kazimoto. Kazimoto anasema kuwa mtu asiyeamini Mungu ni mtu asiyeamua kuwako kwa Mungu kwa kutumia milango ya fahamu peke yake. Baada ya kujipiga risasi, kabla ya kukata roho, Kazimoto anasema kuwa katika maisha aliyoishi duniani, hakupata kukutana hata siku moja na mtu anayeamini kwamba kuna Mungu.

> Unaona Manase, mwanadamu ameamua kuna Mungu kwa sababu ya hali yake ya woga iletwayo na milango ya fahamu. Kwa hiyo mtu anayeamini kwamba Mungu yupo ni yule aamuye kwa kutafuta milango ya fahamu zake. Kwake fahamu zinatawala bongo. (uk 124 )

Kazimoto anakiri kuwa, Kinaya kilichoko ni kwamba utakuta mwanadamu atasali wakati huo huo wengine wanapiga kelele kwamba hakuna Mungu.

> Woga umeleta Mungu, niliendelea kufikiri, na woga umeletwa na mambo yote yanayozunguka mwanadamu. Na ujasiri je, utaleta nini? Nafikiri utaleta kutoamini Mungu. (uk 125 )

Baada ya kifo cha mwanawe, Kazimoto anakufa moyo wa kuendelea kuishi na kuingia katika kilindi cha mawazo. Alianza kufikiri juu ya Mungu; kama kweli Mungu alikuwapo, hakuona kwa nini aliweza kufanya ukatili mkubwa kama huo. Lakini kinyume na usemi wake, Sabina anampa matarajio kwa kumnasihi;

> Mimi nina matumaini bado. Mungu ni mkubwa; anafahamu kila kitu, anatuwekea kitu kikubwa na kizuri zaidi. Anatujaribu kwa mateso ili kuona utulivu wetu.(uk 180)

Wakati wanajadiliana kuhusu ndoto yake, alipoulizwa kama alimwona Mungu, Kalia alimueleza Kazimoto kuwa hakumwona isipokuwa kila wakati walikuw wakifahamu kwamba kulikuwa na nguvu fulani juu yao ambaye alifikiri ndiye Mungu mpenzi. Kazimoto anakiri kuwa, kabla ya kwenda mbinguni lazima tufe.

> Ulimwona Mungu?
>
> Hata! Isipokuwa kila wakati tulikuwa tukifahamu kwamba kulikuwa na nguvu fulani juu yetu, ambaye nafikiri ndiye Mungu mpenzi. Lakini, Kalia, kabla ya kwenda mbinguni lazima ufe. (uk 73 )

Katika riwaya ya Rosa Mistika, tunamwona Rosa akikataa wasia aliokuwa anapewa na padri aliyekuwa amemtembelea kumsaidia Kiroho baada ya kupata habari ya matatizo yaliyokuwa yanamkumba Rosa. Anaamua kuwa mkaidi kwa kila aliloaswa na kubeza.

Wokovu maana yake nini? Wokovu! wokovu gani! Kama kuna moto basi nitakwenda! (uk. 49).

Maneno haya yanadhibitisha kuwa Rosa hakutambua uwepo wa Mungu kwamba angeweza kumbadilisha bali aliamua kuyaishi maisha vile yalivyo. Mambo yanapoenda mrama Rosa anafanya uamuzi wa kukatiza maisha yake. Uamuzi aliochukuwa Rosa ni sawa na ule uliochukuliwa na Kazimoto.

## 2.8 HITIMISHO

Tunapohitimisha sura hii, tungependa kukariri kuwa riwaya hii ya *kichwamaji* ni riwaya ya kifalsafa. Mwandishi E. Kezilahabi anatumia udhanaishi kufafanua matukio kwa ufundi na ustadi wa kiwango cha juu kumwezesha msomaji wake kuelewa dhana ya maisha. Mwanadamu anaishi maisha ambayo yamepangwa kabisa na mwenye nguvu, ambaye wakati wowote anapoamua kuyakatiza maisha yake anafanya hivyo bila kukatizwa na bila taarifa. Yeye ndiye aliye na uamuzi wa mwisho.

Maisha ya mwanadamu yamo mikononi mwake. Mwandishi anatupa suluhisho mbili za maisha haya. Yanapomlemea mwanadamu, anaweza kuamua kuyaishi vile yalivyo kama vile Manase, japo ataishi bila furaha, au ayakatize maisha haya kwa kujiua kama alivyokata shauri Kazimoto. Riwaya hii vilevile, kama tulivyoona kupitia kwa wahusika wake, haswa Kazimoto, inaeleza kwa upana kuhusu uhusiano uliopo kati ya mtu na Mungu, na iwapo mtu anapaswa kuamini kuwepo kwa Mungu.

## SURA YA TATU

## DHAMIRA NA MOTIFU ZA UDHANAISHI KATIKA RIWAYA YA DUNIA UWANJA WA FUJO

### 3.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tunadhamiria kuihakiki riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* huku tukionyesha matukio ya kiusababishi yanayothibitisha dhana ya maisha huku tukiangazia mihimili husika ya kiudhanaishi kama vile ukengeushi, suala la uteuzi, suala la kifo, fujo katika maisha, kihoro na hofu kubwa na kadhalika. Fauka ya hayo, tumehiari kuangazia maozo mbalimbali katika jamii huku tukitoa mifano ili kufanikisha malengo yetu.

### 3.1 SUALA LA UTEUZI

Mbatia, M. 2001: 106) anaeleza kuwa, uteuzi ni istilahi muhimu katika uhakiki wa kimtindo inayorejelea juhudi za kimakusudi za mwandishi kuchagua vipengele mahususi vya lugha na kuvitumia. Mara nyingi, uteuzi huo unatawaliwa na utanzu unaohusika, dhamira inayoshughulikiwa na malengo ya mwandishi kwa ujumla. Mwandishi atachagua kutumia neno, kirai au mpangilio mahsusi ili kuifanikisha sanaa yake. Aghalabu kufaulu au kutofaulu kwa kazi ya kifasihi hutegemea uteuzi wa mwandishi. Kazi bora ni matokeo ya uteuzi wa vipengele vifaavyo wakati na mahali panapofaa.

Uteuzi katika masuala ya kidhanaishi, inamaanisha kufanya uamuzi na kuufuata mkondo Fulani wa tabia au hali. Ni jambo la lazima kufanya uteuzi huu na mbali na kufanya

uteuzi huu, inampasa mhusika awe tayari kuyaona matokeo au mavuno ya uteuzi wake na ayawajibikie, yawe chanya au hasi.

Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo,* mhusika mkuu Tumaini ambaye amelelewa kwa kutendekezwa na wazazi wake mzee Kapinga na Muyango, na kuachiwa mali mengi na pesa ndipo anajitosa mzimamzima katika anasa za dunia, miongoni mwazo ulevi wa kupindukia na kufanya mapenzi na wasichana na wanawake bila kujali. Alifuja mali aliyoachiwa na wazazi wake.

Alipokuwa amejiingiza katika tabia ya kufanya mapenzi na wasichana; anaenda hadi kwa Mugala, nyanyake Leonila, Aurelia, Misana na Dennis ambapo anamwahidi kumletea ugoro kila wakati ili angalau ampe fursa ya kula uroda na Leonila. Tabia hii inapokithiri, tunamuona Leonila akiwa amepata mimba ya Tumaini. Leonila anapodadisiwa kuhusu mimba hii na mamake, Mungere, anakiri jambo hili na kumtaja Tumaini. Tunamwona Leonila akipewa kichapo na babake mzee Kasala anapogunduwa matokeo ibuka ya mchezo huu mbaya. Anamtetea akisema:

> Kasala! Mhurumie binti yako amekwisha haribika. Yeye si msichana wa kwanza kutenda jambo kama hili. (Uk. 21)

Alipohiari kuutafuta ukweli, mamake Leonila anamhoji Anastasia rafikiye Leonola ambaye Leonila alidai kuwa alikuweko siku ya kuingia mimba hiyo. Anastasia anaeleza hali hii kijuujuu bila kujali.

Baada ya maelezo yasiyoridhisha kutoka kwa Anastasia, Mungere anafululiza hadi kwa Tumaini na kumhoji. Tumaini anakataa katakata na kukanusha kuhusika na kitendo hiki kiovu. Alidai kuwa Leonila alikuwa kiruka njia na alihusiana kingono na watu wengi; alikuwa amemsingizia kwa sababu ya pesa alizokuwa nayo.

> Mimi mama Denni, sina hadithi ndefu ya kukudanganya kama ya Leonila – nimekwisha sikia hadithi yake; kwamba nilizoea kutembea na Leonila ni kweli. Sababu zenyewe, mama Denni, ni hizi. Ya kwanza Leonila ni msichana malaya. Ninakuambia uhakika; anafahamiana na watu wengi. Amenichagua mimi kati ya hao kwa sababu ya kisomo changu. Labda pia kwa sababu ya pesa zangu. Pili, nilivyoambiwa na Anastasia anasema kwamba nilimpa mimba tarehe tano, ni uwongo mtupu. Alifahamuje? Jambo linaloshangaza zaidi ni kwamba wakati huo nilikuwa Mwanza. Kwa ufupi ni hivi; mimi sitakubali kumuoa wala kuchukuwa mtoto kabla ya kuona mtoto atakayezaliwa ana pua yangu, macho yangu na rangi yangu! (uk. 8)

Kitendawili kinatokea pale ambapo Anastasia amepindua serikali hii. Anaishia kufanya urafiki na Tumaini hata siku moja walishikwa na mamake Anastasia. Hapa ndipo tunawaona wazazi wa Anastasia wakaamua kumuoza kwa Mzee Tembo bila pendo lake. Mzee Tembo alikuwa amemuoa Balizunaki dadake Anastasia lakini akaaga dunia. Ilitarajiwa kuwa Anastasia aolewe na mzee Tembo ili aende alee watoto wa dadake mwenda zake, ambao ilidaiwa kuwa wanateseka na pia kama njia moja ya kutowa shukrani kwa sababu mzee Tembo huwasaidia sana familia ya Kasala kwa hali na mali ili kukidhi mahitaji yao. Anastasia anakaidi wasia huu na anahiari kumweleza Tumaini ili

apate ushauri. Tumaini anachekelea sana jambo hili na kumwambia kwamba atamueleza vile watawafunza wazee wenye tabia ya kuwaoza mabinti zao bila ya hiari yao. Anapojulishwa na Anastansia maendeleo ya mtoto wake tumboni mwa Leonila. Tumaini anakejeli na kufoka:

> Usiseme mtoto wangu. Mtoto wangu wa kwanza atoka tumboni mwako. Usiniambie habari za Leonila. Hukusikia ninawambia kwamba mtoto atakayezaliwa wanaweza kumtupia mbwa. Kama hawataki wanaweza kumpeleka kwa mama Huruma atunzaye watoto yatima. (uk. 41)

Sadfa inayotokea hapa ni kwamba, wakati huohuo Tumaini naye alikuwa amezongwa na matatizo kuhusu tabia yake ya kuwaharibu wasichana na hivyo kughadhabisha wakaazi wa kijiji cha Bugolola na hivyo kichwa kilimwanga afanye nini. Vilevile alikuwa amekerwa na kitendo cha kuwaona wazazi wake wakiwa uchi ambao japo walikuwa wamekufa, walikuwa wamekuwa vizuu. Kila mahali walipoonekana, jina lake lilitajwa. Tumaini alimueleza Anastansia njama yao ya kutorokea mjini. Anastasia alikuwa aombe ruhusa ya kwenda kushiriki katika ngoma zilizokuwa siku chache kabla ya Harusi yake na mzee Tembo kisha watoroke ngomani. Tumaini anamweleza Anstasia:-

> Hata mimi mwenyewe nina shida karibu na yako. Sipendi kuwaona wazazi wangu wakitembea uchi; ni fedheha kwangu. Iliyopo ni kuhama tu na tutahama pamoja. Siwezi kukuacha nyuma".
>
> "Tutakwenda wapi? Anastasia aliuliza. "Nchi za mbali" "Mwanza". Huko ndiko nasikia kuna maisha. (uk. 43)

Dondoo hii inatuonyesha ile hamu na ghamu aliyokuwa nayo Tumaini ya kuyafurahia maisha haya ya mjini. Alifaulu kutoroka na Anastasia kama walivyopanga; akayaparamia maisha ya mjini yaliyomngoja kwa mikono miwili kummeza; naye akamezeka. Maisha aliyotarajia hakuyapata, ila maisha masumbufu, yenye maumivu na mateso yanayoisha katika kupoteza maisha kwake kama tunavyoona mwisho wa riwaya. Tumaini ni ushahidi tosha wa vile mwanadamu anavyojitahidi kupata furaha katika maisha bila mafanikio, uteuzi anaofanya hivyo basi unamwingiza katika maangamizi yasiyopimika. Kule nyumbani sherehe na mipango ya harusi ya Anastasia iliendelea kama ilivyopangwa lakini Bi Harusi katoweka na hivyo kumuacha mzee Tembo na wazazi wake wakiwa wameshika tama.

Uteuzi wa Anastasia kumpokonya Laonila mpenzi wake tunaona matokeo yake katika sura za mwisho za riwaya yenyewe. Kitendo alichofanya hakikumpendeza hata yeye mwenyewe. Tunamwona akimdadisi Tumaini ili kuhakikisha kama ataolewa naye.

> Tumaini utanioa? Kwa nini unaniuliza swali hilo? Leonila Je! Mara ngapi nimekwambia kwamba Laonila sinaye haja tena isipokuwa wewe). (uk 24).

Anastasia alifikiri kwa muda. Wakati ulifika wa kuvunja urafiki na Leonila kwa kumnyang'anya mpenzi wake. Anastasia alifikiri sana, lakini yeye pia alikuwa na matatizo yake. Baadaye, Leonila anasafiri mjini na kumpeleka mtoto aliyempata na Tumaini. Hivyo basi, Anastasia alikumbwa na jukumu la kumlea mtoto huyu hivyo basi kuwajibikia vitendo vyake vya kumpokonya mwenzake mchumba wake.

Kwa mujibu wa wanaudhanaishi, binadamu anajikuta katika hali ya maisha ambayo ni kama mtego. Ulimwengu wenyewe hauna maana. Kwanza, kwa sababu binadamu

anakabiliwa na tatizo la uhuru. Huu sio uhuru wa kufurahisha bali wa kuogofya na kutisha. Hamna kitu cha kumsaidia katika kuutumia uhuru wake huo au kuufanya uchaguzi ambao hana budi kuufanya. Binadamu huyo hana njia pia ya kuyakwepa madhara yanayotokana na uchaguzi atakaoufanya.

Tukio la Kasala kumpiga Leonila lilimuudhi sana nyanyake Leonila, Mugala ambaye ndiye aliyekuwa anafaidika kwa zawadi za ugoro kutoka kwa Tumaini ili kuwaacha wajukuu hawa kuburudika na wavulana. Kasala aliyekuwa anafahamu jinsi mipango hii ilivyokuwa inaandaliwa, alimfokea mamake na kumwambia.

> Kwa nini unaniharibia binti zangu! Unakubali kudanganywa kwa ugolo! Lini uliniomba ugolo nikakunyima! Mugala alikataa kula. Alikwenda kulala akiwa na hasira kubwa. Hata kama mkinikataaa nikifa mbwa wangu atanila (uk 22).

Mugala atoroka, apotea. Kasala anapatwa na kibarua cha kumtafuta mamaye. Anapofika mtoni akaona nguo ya mama yake ikielea majini juu ya majani; pembeni akaona fimbo. Kasala alifahamu Mugala kachukuliwa na mkondo wa maji alipokuwa akivuka. Alitaharuki, akakaa chini na kuanza kufikiria, huku akilalama;

> Mama, kama ningefahamu nisingekuambia neno lolote! Umekufa! Umekufa kwa sababu ya ujinga wangu. Umechukuliwa na mto kwenda kuliwa na samaki ziwani kama kwamba hukuwa na jamaa! (uk. 22).

Hapa tunamwona Kasala akiwa anajutia uteuzi aliofanya wa kumfokea mzazi wake. Mugala mamake Kasala na nyanyake Leonila, alituhumiwa kuwa mchawi aliyekuwa na uwezo wa kugeuza watu kuwa vizuu. Vizuu hawa hutumika kulima mashamba ya bwana zao wakati wa usiku. Mara nyingi hutunzwa juu ya dari au machakani. Tumaini

alipojileta mwenyewe kwa Mugala ili afanyiwe mpango na kuondoka na Leonila usiku usiku, Mugala alibaini kuwa amepata njia rahisi ya kuyanasa mawindo yake. Alidai kuwa jamaa zake Tumaini ndio waliokuwa wamehusika na kifo cha bwanake kwa kumfunga jiwe shingoni na kumtosa majini; hivyo alikuwa amefanya uamuzi wa kulipiza kisasi kwa kumuua Tumaini. Lakini, Mugala anaamua amuache Tumaini afanye mapenzi na Leonila kwanza, ndipo atekeleze malengo yake. Uhusiano huu wa wapenzi hawa wawili; Leonila na Tumaini ndio unamfanya Leonila amfichulie siri kwamba wazazi wake walikuwa wamegeuzwa vizuu na Mugala. Leonila alisikika akimwambia Tumaini:

> Tumaini unafahamu nakupenda sana Tumaini nipende mimi wakati huu ungalikuwa unalima mashamba bure. Baba na mama yako wamo ndani ya chaka karibu na nyumbani kwetu. (uk.20).

Katika ufichuzi huu, na kesi iliyozungumzwa kwa mwanangwa, Tumaini na Anastasia wanatoa ushahidi. Uamuzi unapitishwa kuwa Mugala ahamishwe hadi kisiwa cha wachawi karibu na kisiwa cha Ukerewe. Hivyo basi, shabaha yake ya kumkatiza Tumaini maisha yake haikufaullu kwa ajili ya uteuzi aliofanya wa kumhurumia Tumaini kinyume na kiapo alichokula kuwa hatamhurumia mja yeyote.

Makoroboi ndivyo alivyojulikana pwaguzi kutoka mjini aliyekuja kijijini Bugolola kuibia watu nguo na pesa. Yeye ni mhalifu maanake siku moja alionekana akiuzia watu nyama za binadamu alizokuwa amezichoma mshakiki. Watu walimzigira na kumtoa katika maficho yake; anapigwa na watu baada ya kutukanwa na kutemewa mate. Anapata majeraha mabaya na baada ya hayo akaenda korokoroni kufunzwa adabu njema na

kurekebisha ukosefu wa maadili alionao. Uteuzi aliofanya wa kuibia watu ulikuwa umemwingiza matatani. Makoroboi anakutana na Tumaini wakati akifukuzwa na umati wa watu. Kama si Tumaini kuwaonyesha watu alipo, hawangemuona. Tunamwona akimbembeleza Tumaini asimseme, maanake alijuwa matokeo ya kupatikana.

> Rafiki yangu ninakusihi usinipigie mayowe! Yule mtu alimwambia Tumaini kwa upole. (uk. 44).

Mwishowe walimuona. Yule mtu alitupa kisu chake chini na kukata tamaa. Tumaini alipomkomboa alimtandika fimbo begani na kumwangusha chini; alianuka na mzigo wake. Walipokutanisha macho, Tumaini alikumbuka vile ambavyo mtu yule alivyokuwa amemsihi. Wakati huo, Tumaini alikuwa kijijini Bugolola. Alipohiari kuhama mjini, anakutana tena na Makoroboi. Wakati huo, Tumaini kaajiriwa kufanya kazi ya upelelezi katika mabaa. Njama ilifanywa Tumaini apigwe na aliyepewa kibarua hicho kwa kulipwa pesa ni Makoroboi. Mpango unafanywa kuwa mwanamke anayeitwa Kristina anajifanya kumpenda Tumaini kwa baa na kuenda naye kwa nyumba yake; naye Makoroboi na wenzake kumpiga Tumaini na kuharibu sura yake.

Makoroboi anamuuliza Tumaini kama anamkumbuka na kumuonyesha Tumaini alama iliyofanywa na ile fimbo aliyompiga siku ile. Wakati huo Makoroboi kamaliza kifungo chake. Wakati huo, Tumaini alijutia uteuzi wake wa kumsema, kumpiga na kumpigia makelele Makoroboi siku ile kule Bugolola maanake sasa alipata nafasi ya kulipiza kisasi.

Alipofikia umri wa kuoa, Dennis alipata mwanamke aliyeitwa Vera. Baada ya kufanikiwa kumpata kifungua mimba wao, sasa alijulikana kama mama Resi. Mwanamke huyu anaonekana mzembe sana na mwenye kujipenda na kupenda starehe. Tunamuona akiwa safarini ndani ya gari lililoharibika, abiria wote wanashuka lakini yeye anakatalia ndani. Jambo linalomfanya afinywe mdomoni na vyuma na ngeu kumtoka. Yeye na Dennis ni mfano mzuri wa ndoa za kisasa, ndoa za wasomi; wanaofuata utamaduni wa kizungu na kupuzilia mbali utamaduni wao wa Kiafrika. Siku moja, Dennis alifika kwake, yuahisi njaa, badala ya mama Resi ampe chakula, alimwonyesha kwa mguu:-

> Basi, mwenzetu Dennis alipofika nyumbani alimkuta mke wake (wa mbali) amelala kitandani. Dennis alipoomba ugali, mke wake alimwonyesha kwa mguu-ule pale mezani – alifokewa – unakunywa pombe ya kienyeji, leo hulali nami (uk. 36).

Mama Resi anafanya urafiki na John, rafiki ya Tumaini. Uhusiano huu unaanzwa na mama Resi mwenyewe wakati Tumaini na John walikuwa wamemtembelea. Uhusiano huu unaponoga, tunamwona mama Resi ataka John amuite Vera.

> Usiniite mama Resi; wewe uwe unaniita Vera. Vera ndilo jina langu halisi. Ndio jina litumiwalo na wapenzi wangu. Nasikitika kuona kwamba siku hizi silisikii mara nyingi. (uk. 85)
>
> Hata kama Dennis akifahamu, hana matata maskini (uk. 86)

Jambo hili liliendelea kwa muda. Japo mumewe anaporejea, ndivyo mama Resi alivyoonyesha mapenzi zaidi kwa mumewe, huku akitandika kitanda vyema. Hata wakati alipoingia chumba cha kulala alikuta chumba chote kinanukia manukato. Juu ya kitanda

aliona ua la waridi. Mto uliokuwa umepambwa kwa maandishi ya "Welcome Back" ulikuwa umewekwa juu.

Siri hii inafichuka pale ambapo mama Rasi anaamua kwenda kumdunga Tumaini kisu kwake nyumbani lakini akafeli. Awali, mama Resi, mwenye Africans' Royal Bar, Makoroboi na Kristina walikuwa wamefanya njama ili Tumaini "afunzwe adabu." Lakini yeye mama Resi alitarajia Tumaini auawe. Tendo ambalo Makoroboi hakufanya. Alimchukia Tumaini kwa sababu tatu. Kwanza, aliona yeye alikuwa kizuizi kwa John kufika kwake ili afanye mapenzi naye. Pili, aliona Tumaini alikuwa amekuwa maarufu sana mjini kuliko Dennis, kwa sababu Tumaini sasa alijulikana kama "mwenyewe". Tatu, Tumaini alionekana mwerevu kuliko Dennis katika majadiliano na majibizano mbalimbali. Mwenye baa naye alikuwa na chuki kwa sababu kufuatia kazi yake ya upelelezi, ilifikia kwamba tumaini akiingia kwa Baa wateja wanatoroka na hivyo mwenye baa hakupata faida ya biashara yake. Alipofika kwa Tumaini, hasira sasa ilizidi kwa sababu hawara wake John, alikuwa amefurushwa na Tumaini kwa kutofanya kazi na kile Tumaini alichokiita kuingiliwa kwa nyumba yake na John.

> Mama Resi usiniudhi kwa maneno yako machafu. Kama unamtaka hawara wako, nimemfukuza sasa unataka nini zaidi? Tumaini alisema kwa hasira.

Alipokosa kufaulu kumdunga Tumaini kisu, anarudi kwake na kumkuta bwanake ameingia kutoka kazini, anatunga uongo na kusema kuwa karibu Tumaini amnajisi. Dennis anangurumisha gari moja kwa moja hadi kwa Tumaini na hapo ndipo alipoelezwa yaliyojiri kati ya mama Resi na John. Hapo ndipo Dennis alipokula mori na kumpa mama Resi talaka. Alikuwa na ushahidi wa kutosha kuhusu vitendo vya mke wake kukiwemo

mkutano waliofanya wa njama ya kummaliza Tumaini. Barua iliyoandikwa na mama Resi kwa mumewe wa zamani Dennis inaonyesha majuto na kunyenyekea kwa hali ya juu. Anaomba nafasi ya kuruhusiwa angalau awe anaruhusiwa kuenda kumtazama mtoto wake Resi. Hatimaye Dennis alihiari kuoa mke mwingine; Bernadeta. Hayo ndiyo yaliyokuwa matokeo ya uteuzi aliofanya mama Resi ya kufanya mapenzi nje ya ndoa.

Ukosefu wa maadili miongoni mwa vijana umewatumbukiza katika majanga kadha wa kadha humu duniani. Kasoro hii inawafanya kufanya uteuzi ambao bila shaka umewagharimu, kiasi cha kugharimu maisha yao. Vijana wawili katika ngoma walifumaniwa wamelala katika kichaka ambamo kila mtu aliweza kuwaona. Kitendo hiki kilichukuliwa na wanadamu kama madharau. Hawakuthamini wenyeji wao ili watimize haja zao za kimwili.

> Piga! Piga! Ua! Piga mbwa!
>
> Watu wengi walikimbia kwenda kutazama kulikuwa na fujo gani. Tumaini, Anastasia na John pia walikimbia kuenda kuona. Na pale katikati ya kundi la watu walikuwa wamelala vijana wawili; kijana na msichana. Damu ilikuwa inawatoka puani. Kusema haki vichwa vyao vilikuwa vimepasuliwa kwa rungu. Walikuwa wamekufa. Pale katikati walikuwa wamelala mfano wa wanyama, kama mbwa (Uk. 50).

Tunawaona vijana hawa wawili wakiwajibikia uteuzi waliofanya wa kutaka kukithi mahitaji yao dhidi ya heshima wanayostahili kuwa nayo.

Akiwa Shinyanga, Tumaini japo walikuwa sasa wameoana na Anastasia, alikuwa na uhusiano na viruka njia; haswa wanawake waliofanya kazi katika Africans' Royal Bar.

Aliyehusiana zaidi ni Hadija. Wakati mmoja, Hadija anaamua kumtembelea Tumaini nyumbani kwake ili ajuwe kiini cha Tumaini kutofika kwake usiku usiku kama ilivyokuwa mazoea yake. Vilevile, alitaka msaada wa fedha. Maanake hata mwenye nyumba alidai kodi ya mwezi. Kitendo hiki kilimuudhi sana Anastasia aliyeamua kuchukuwa ukuni na kumgonga nao Hadija kichwani huku akifoka:

> Malaya wewe! Toka! Hapa! Wewe ndiye unatuambukiza magonjwa!" Anastasia aliendelea kumpiga tena na tena kama mtu apigae nyoka. John na Tumaini walipokumbuka kumshika Anastasia, Hadija alikuwa amekwisha haribika sura.
> Acha nimuue! Mshenzi! Hii ni dharau kubwa sana! Malaya hawezi kuja kuzungumza mambo yake na bwana wangu mbele yangu! Waziwazi namna hii! Ala! (uk. 84).

Alipoamka, Hadija japo alikuwa ameharibika sura, aliwashangaza Tumaini na John, maanake alitoa bastola na kumfyatulia Anastasia ambaye alianguka chini huku Hadija akikebehi.

> Mtoto wa mbwa! Unafikiri bwana wako ana nini! Anakupa nini ambacho mimi sipati! Hufahamu kwamba pesa za bwana wako huwa tunagawana!

Wakati huo, Anastasia alikuwa amelala juu ya sakafu kama maiti. Wakati Tumaini alitaka kumpokonya Hadija bastola; Hadija aliamuru;

"Ala! Simama hapo ulipo! Sasa nataka jambo moja tu! Funguo za sanduku hili! Upesi! Shinyanga hii, ndugu zangu! Mara hiyo risasi ilipasua suruali ya Tumaini na kumkwaruza mguuni. Wote sasa walikuwa mateka wake na alifanya anavyotaka bila tashwishi.

Mara ya mwisho upesi! Kabla sijafyatua!

Tumaini kwa kuokoa maisha yake yaliyokuwa hatarini, alipeana funguo naye Hadija akalipekuapekua na kuiba shilingi elfu moja. Kutamatisha na kudhibitisha ujambazi aliokuwa nao, aliwapiga Tumaini na John risasi za miguuni na kuwaacha wamelala juu ya sakafu wakilia kwa maumivu. Aliyepaswa kulaumiwa kwa majeraha na hasara iliyopata familia hii ya Tumaini ni uteuzi wa Anastasia wa kumtukana na kumvamia kwa ukuni; Hadija naye akaonelea ajitetee na kuwafunza adabu.

Mwanaudhanaishi Jean-Paul Satre (1975) anamtazama binadamu kama mwenye kuwajibika kwa matendo yake lakini mwenye upweke katika uhuru unaoogofya wa kuchagua na kujiendeleza katika ulimwengu usiokuwa na maana.

## 3.2 UKENGEUSHI KATIKA DUNIA UWANJA WA FUJO

Wamitila, K.W. (2003: 285) anaeleza kuwa, ukengeushi ni istilahi ambayo inajitokeza sana katika tahakiki na uhakiki wa fasihi. Katika uhakiki wa ki-Marx dhana hii juwa na maana ya hali ambayo mfanyikazi anachangia katika uzalishaji mali katika mfumo wa kibepari lakini kuishia kuwa mbali na matokeo ya juhidi zake. Katika uandishi wa ki-usasa na ki-usasaleo dhana hii hutumwa katika upana wake kuelezea hali ya kubaguliwa pamoja na upweke unaohusishwa na fasihi ya aina hiyo.

*Encyclopedia Britanica* (1958) inasema kuwa ukengeushi ni ile hali ya kuhisi ugeni au utengano kutoka kwa kazi yako na hatimaye mazao ya kazi yako. Kulingana na maelezo haya, tunaweza kuorodhesha ukengeushi kuwa ule wa mtu na watu wengine, mtu na jamii yake na hatimaye ukengeushi wa mtu na nafsi yake mwenyewe ambao tunaweza kuuita ukengeushi wa kisaikolojia.

Katika riwaya hii ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, tunamwona mhusika mkuu Tumaini akiwa amekengeuka kulingana na matukio ambayo yanadhihirika waziwazi. Kama vile katika riwaya ya *Kichwamaji*, matukio haya yanaonekana kutokea kiusababishi. Tukio moja la awali linalonekana kusababisha lingine.

Anastasia anahama mjini na Tumaini ili kuepa harusi yake na mzee Tembo; umri wa babake ambaye alikuwa amemuoa marehemu dadake, Balizunaki. Mzee Tembo alisaidia familia ya akina Anastasia kifedha; alikuwa tajiri. Anastasia alimchukia mzee Tembo kwa uzee wake. Tumaini aliuliza;

> Baba yako amepanga mpango gani?

> Wamepanga pamoja na Tembo kwamba atanioa siku ya Jumatatu baada ya majuma mawili, maskini sijui nifanye nini! Hakika sitaweza kumvulia nguo mzee anayelingana na baba! Sijui nifanye nini nipate kuepa fedheha hii! Anastasia alilia. (uk. 42).

Tumaini naye alimpa matumaini na kumhakikishia;

> Anastasia usilie, lazima tuwaonyeshe wazee kwamba mpango wa zamani umekwisha. Huu ni ulimwengu wa ndoa za mapenzi; siyo tena ulimwengu wa kugawa mabinti kama zawadi kwa watu wasiowapenda. (uk. 42).

Njama yao ya kutoroka kwenda mjini na Tumaini ilifaulu. Kwa kutoroka huku, Anastasia alikaidi mila, desturi na utamaduni wa jamii yake. Isitoshe, kutoroka ilimaanisha kukengeuka au kutengana na familia yake. Penginepo ingewafaa watoto wa dada yake waliokuwa wanateseka kwa sababu baba yao alikuwa mzee na hangeweza kufaulu kuyafanya majukumu yote ya unyumba. Heri angakataa kuolewa na mzee Tembo na kubaki kwao, na kuendelea kuwafaaa wazazi wake, lakini hatua ya kutorokea mjini na Tumaini na kuwa kimada ni hasara pande zote, kwao na kwa dadake marehemu aliyekuwa ameacha watoto watatu alipopiga dunia teke.

Hatua ya kumuoza Anastasia kwa mzee Tembo iliharakishwa na kuafikiwa na wazazi wake hasa baada ya kufumaniwa na mamake wakifanya ngono na Tumaini. Alipotoroka, Mulele na mke wake walianza kumtafuta kwa machozi na kulaumiana kwa sababu tayari walikuwa wamefanya sherehe nzuri sana. Walibabaika sana waliposikia kuwa kuna vijana wawili waliouawa na watu pale ngomani walipofumaniwa wakifanya mapenzi.

Walihofia kuwa pengine hao ndio walikuwa wameuawa. Tunamuona mzee Mulele, babake Anastasia akifoka;

> Babu atafufuka kama msichana huyu asiporudi kwangu! Jua linitege mgongo! (Uk. 52).

Alipojikengeusha na familia yake (uk. 55), tunamwona Anastasia huku akivuka boti kuelekea Mwanza akiwaza na kuwazua, juu ya rafikize Leonila na Aurelia wakiwa wanaenda kusali. Jambo hili lilimkosesha furaha na kumletea masikitiko na majonzi.

Katika riwaya hii, tunamuona babake Tumaini mzee Kapinga akiwa hashirikiani na jamaa zake akiwa hai. Anapokufa, watu wachache sana wanahudhuria mazishi yake. Inasemekana kuwa kama si watoto wa shule waliokuja kwa ajili ya mwenzao Tumaini, kaburi lake lisingalikwisha kuchimbwa. Watu walisikika wakisema:

> Pesa zake zitamzika.

Wengine walisema, wema wa mtu hujulikana siku ya mazishi. (uk.13). Hayo ndiyo yaliyokuwa matokeo ya utengano baina ya babake Tumaini na jamii yake.

Kulingana na utamaduni wa Kiafrika, mwanamke anapaswa kumshughulikia mume wake pale inapohitijika. Ni katika utamaduni wa Kizungu tu, ambapo majukumu ya unyumba yanagawanywa kati ya Bwana na Bibi. Elimu ya kimagharibi vilevile imeathiri kwa kiasi kikubwa familia za karne hii na kusababisha watu ninaoweza kuwaita "Wazungu weusi". Tunamuona mke wa Dennis, mama Resi (Vera) akiwa ametoka safari na anapofika

nyumbani, japo wageni wapo, anamueleza mume wake kuwa amechoka; na anaenda kulala; hivyo basi Dennis alipaswa kuwatayarishia chakula. Bila dukuduku wala upinzani, Dennis anafanya hivyo.

> Utawapikia wageni nini? Aliuliza. Nimechoka na safari, nakwenda kulala tu. (Uk. 59).

Mambo yanayotokea hapa ni sawa na yale tunayoyaona katika riwaya ya *Kichwamaji.* Salima mkewe Manase hakuweza kuamka asubui na mapema ili kumtayarishia mumewe na wageni kiamshakinywa bali alimngoja mzee aliyekuwa mpishi wake hadi pale alipowasili, ambaye alifika kuchelewa, jambo lililoleta mtafaruku baina ya Salima na mpishi huyo.

Kwa maoni ya wanaudhanaishi, kiumbe ambaye amekengeushwa na nafsi yake, na anayekuta katika umati mkubwa na alazimikaye kufanya uteuzi fulani, anaishia kuwa katika hali ya dukuduku. Hili ni suala linalojitokeza katika kitabu cha Kierkegaard kiitwacho *Fear and Treambling.*

## 3.3 KIHORO, HOFU/DUKUDUKU KATIKA RIWAYA YA DUNIA UWANJA WA FUJO

Kulingana na wanaudhanaishi, binadamu anajikuta katika mseto wa hofu na wasiwasi, inayomfanya ashindwe kujua la kufanya. Mwanaudhanaishi Martin Heideggar alisema kuwa binadamu ana hiari na matukio maishani mwake ambayo mara kwa mara yanakuwa kama ajali. Athari na imani hii inatokana na madai ya Haeideggar kuwa binadamu anashurishwa kutegemea ajali, wazo ambalo hujaribu kulitoa mawazoni mwake, lakini haliwezi kuikwepa hali hii kwa vyovyote vile. Motifu ya ajali imetumilka kutudhihirishia kuwa binadamu hana chochote ambacho anaweza kujipangia. Matukio yote maishani mwake ni ajali tu.

Jambazi sugu katika riwaya hii Makoroboi alipopatikana na hatia ya kuiba pesa na nguo, alifungwa. Hata hivyo, anamaliza kifungo chake na kurudi mjini kuendeleza uhalifu wake. Kwake yeye, akipewa hela, alikuwa tayari hata kukatiza maisha ya mtu. Makoroboi alipewa pesa na mwenye Africans' Royal Bar na mama Resi ili "amfunze adabu" Tumaini. Kulingana na mama Resi, alitaka Tumaini auawe; jambo ambalo Makoroboi hakufanya kwa sababu hawakuwa wamekubaliana hivyo.

Baada ya njama hii kujulikana, mama Resi alitaka kumpa Makoroboi pesa ili aende amalizie kazi hiyo lakini yeye alizikataa; hata aliporushiwa alighairi kuzichukuwa kwa hofu ya kushikwa. Alijitetea kuwa alifahamu wanasakwa na ilimlazimu kutoroka haraka iwezekanavyo pamoja na wenziwe waliokuwa wametekeleza uhalifu huo. Katika mkutano huo, mama Resi asema:

Mimi nilifikiri kwamba mpango huu ulikuwa wa kumua!

Hapana sisi tuliambiwa kumfunza tu, basi,

Angalieni sasa tumo matatizoni. Huenda tukanyongwa au kufungwa maisha!"

Mama Resi alisema maneno hayo kwa kelele.

Sasa tumo taabuni, Makoroboi alisema, Polisi wanatusaka mimi na wenzangu.Tutaondoka mjini kwenda nchi za mbali, na hatutarudi tena kabla ya miaka miwili kupita (Uk 98 – 99).

Baada ya Mugala kufukuzwa kule Bugolola kwa ajili ya vitendo vya kichawi, naye Tumaini alikwisha zomewa kule kwa Mwanangwa, alikuwa na hofu kuwa pengine hata yeye watu walimchukia na kumkasirikia kwa tabia ya kuharibu Binti zao. Tumaini alifikiri:

> Mugala alipigwa na watoto wadogo, alitemewa mate, lakini hata jamaa zake walimtazama tu. Kumbe raia wakikususa unakuwa kama mnyama! Mimi je? Huenda labda watu wamekwishaanza kunikasirikia kwa kuharibu binti zao! Kuna mambo mawili ninayoweza kufanya; au nirekebishe mwenendo wangu na niendelee kuishi humu kijijini au nitoroke niende nchi za mbali kabla mtumbwi haujatoboka. (uk. 32).

Wazazi wa Tumaini ambao walikuwa vizuu, walimfanya aone fadheha kwa vile walikuwa wakitembea uchi. Jina lake lilitajwa kuwa ni mtoto wao kila mahali walipoenda. Alipokuwa anaulizwa kama ni wazazi wake, alianza kuwakana. Alianza kuona aibu juu ya wazazi wake hivyo basi akaanza kutafuta njia ya kuepa fedheha hii.

(uk. 33).

Jaribio la mama Resi (Vera) mkewe Dennis la kumuua Tumaini lilipofeli, aliporudi nyumbani kwa mumewe ilimbidi adanganye kuwa Dennis alitaka kumnajisi. Baada ya mumewe kumsikiza kwa makini na kuwazia mambo haya, aliamua kuenda kwa Tumaini kupata ukweli wa mambo. Kipindi hicho kilikuwa kigumu sana kwa mama Resi kwa sababu alijawa na hofu kuu kwamba pengine Dennis akifika huko ataambiwa ukweli wa mambo, na pia ajulishwe vile ambavyo yeye (Mama Resi) alikuwa akizini na John. Wasiwasi aliokuwa nao uliishia yeye kupewa talaka maanake Tumaini hakusita kupasua chungu na kutoboa kila kitu.

John, rafikiye Tumaini kutoka kijiji cha Lutare, waliyeondoka pamoja kuelekea mjini alionyesha hulka za kustaajabisha sana. Baada ya wao kuponda mali na kuishiwa, Tumaini anaamua kuwa mkulima. Analima kwa bidii sana huku akimwacha mke wake nyuma akiendelea na majukumu ya nyumbani. La kustaajabisha ni kwamba, John naye barubaru mwenye nguvu tele alihiari kubaki nyumbani pamoja na Anastasia. Tendo hili linaendelea kwa muda mrefu hadi pale ambapo siku moja Tumaini aliporudi kutoka shambani anamfumania John katika chumba cha Anastasia afanya nini? Ati alikuwa akicheza zile shanga. Alipoona vile, Tumaini sura iligeuka. Alionyesha kuwa na hasira na hapo akashuku kuwa huenda John akawa amemzunguka mbuyu na sasa alikuwa akimla kivuli John naye alijitetea akasema:

> Tumaini, nilikuwa nikicheza kidogo na shemeji. Nilikuwa nikimuelezea kuwa siku hizi unampenda sana. Nilikuwa namwambia kwamba mapenzi hayo ndiyo yamefanya ukaacha kwenda kunywa pombe mjini. (uk. 105).

Tukio hili linatosha kumfanya Tumaini kuwa na hofu kuwa sasa mke huyu alikuwa ni wao wote. Barua aliyoandika na kumpa John wakati akimfurusha arudi kwao Lutare inadhihirisha haya. Mambo aliyosema kwa uzito na tahadhari yanamwacha msomaji na maswali chungumzima. Hakuna jambo linalouma moyoni kama kugawana mwanamke na mabwana wengine na hakuna mtu anayekudharau kama yule afahamuye siri zote za mkeo (uk. 106).Anastasia naye kwa upande mwingine alipata kihoro alipoona kuwa mumewe amekataa hata kula chakula cha mchana.

Katika pilkapilka zake za kuenda baa na kustarehe, siku ile ambapo Tumaini alikuwa ameundiwa njama afunzwe adabu alikutana na Kristina ambaye baada ya kulewa, walikodisha tekis na kuenda kulala mahali ambapo Kristina alidai ni kwake huko Maganzo. Walipoingia chumbani, Tumaini anaona suruali ya mwanamume imetundikwa ukutani. Akamuuliza Kristina:

> Suruali hiyo ni ya nani?
>
> Ni ya bwana wangu," Kristina alisema.
>
> Unafikiri mimi mjinga kuleta bwana mwingine na hali bwana wangu yuko nyumbani! (Uk. 95).

Tumaini alikaa, lakini moyo wake ulikuwa na hofu kubwa kila wakati. Aliposikia kitu fulani kama panya, aliamka mara moja kwa woga.

> Sijaona mwanamume mwoga kama wewe! Kristina alisema. (Uk. 96)

Hivi ndivyo siku Tumaini alipigwa na kuharibiwa sura na Makoroboi na wenzake mpaka akazirai.

### 3.4 UKATAJI TAMAA KATIKA DUNIA UWANJA WA FUJO

Udhanaishi ni falsafa inayokatisha tamaa (inatamausha) kwa sababu haitoi mwanga kuhusu uwezekano wa hali kubadilika na kuwa nzuri zaidi. Tena ni nadharia ya kibinafsi inayomtafakari binadamu katika upweke wake. Kwa mujibu wa mdhanaishi Jean-Paul Satre, mtu huzaliwa au hujipata ametumbukia kwenye ombwe fulani. Yuko huru kuishi tu katika ombwe hilo au kuishi huru akikabiliana vilvyo na ulimwengu uliomzunguka. Kwa kuwa hana uwezo juu ya masuala kama maumivu na mateso, anaweza kukata tamaa.

Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fuj*o, kuna matukio mbalimbali yanayodhihirisha ukataji wa tamaa. Mzee Tembo ambaye mke wake Balizunaki kaaga dunia, alikuwa ameahidiwa na wakwe zake kuwa Ataozwa Anastasia. Anaamua kufunga pingu za maisha na Anastasia – baada ya kulipa mali iliyokuwa inatakikana. Baada ya matayarishio kemkem ya Harusi, siku chache kabla ya harusi yenyewe Ansastasia anatoroka na Tumaini na kuelekea mjini. Katika ziara zake za kuendeleza uchumba wake, anapopewa nafasi kuongea naye kule jikoni anaonekana kumtamani, alimpapatikia na kummezea mate. Alijaribu kumshawishi na kumrai kuwa watoto wa dadake wanateseka nao walihitaji uangalizi wake. Wazazi wa Anastasia walijaribu kila njia kumfanya ampende mzee Tembo bila mafanikio. Alipokuja kwao, Anastasia aliulizwa kumpokea fimbo na alipokuwa anaondoka, vilevile aliulizwa kumsindikiza.

Haya pokea fimbo yake. Peleka ndani ya nyumba. Anastasia alipokea mikono miwili hali akipiga goti moja chini. Muda wote Tembo alikuwa akimwangalia msichana atakayekuwa mke wake kwa hamu kubwa. Aliyaona machuchu, alikiona kiuno chake.

Tembo alitamani mtoto wa watu. Hata alipokuwa amekaa alikuwa akijilamba ulimi mara mbili kila wakati alikuwa akitupa macho jikoni.

> Naam! Bila shaka umemwona mara nyingi. Siku hizi amekua. Nimemwona. (uk. 39)

Alipomkosa Anastasia, Mzee Tembo aonekana kukata tama. Alikuwa amemkosa ndege wake aliyemwinda siku nyingi.

Katika harakati za kuokoa maisha yake baada ya wizi aliohusika nao, Makoroboi alijificha mahali ambapo mtu aliyejuwa ni Tumaini pekee. Alimsihi Tumaini asimpigie makelele na kumwambia:

> Rafiki yangu ninakusihi usinipigie mayowe! (uk. 44).

Baada ya kusema hayo, aliingia ndani ya shamba la mihogo. Lakini Tumaini alifichua siri huku akiwaambia umati wa watu waliojawa na hamaki.

> Ameingia humu! Nimemwona!

Tumaini aliwambia watu hali naye ameshika fimbo mkononi. (uk. 44).

Baada ya kusema haya, shamba lote lilizungukwa mara moja. Mwishowe walimwona, Makoroboi alitupa kisu chake chini kama ishara ya kusalimu amri kwa sababu kisu chake kimoja hakingefanya chochote dhidi ya silaha za kila aina zilizokuwa zimebebwa na wafukuzaji. Yeye alikata tamaa na akafahamu kuwa mbio za sakafuni huishia ukingoni. Alitiwa nguvuni, na kufungwa gerezani.

Baada ya Tumaini kupatwa na mkasa wa kupigwa hadi kuzirai na kuharibiwa sura, anabahatika kutupwa karibu na hospitali. Alipata matibabu kwa muda kabla ya kutolewa. Akiwa hospitalini, Anastansia na John walimtembelea kujua maendeleo yake na vilevile kumliwaza. Walipoingia, Tumaini alianza kulia. Alionekana kukata tamaa na hakutaka kusikia chochote juu ya maisha. Alisema:

> Msinizungumzie tena juu ya maisha. Tumaini alisema msinizungumzie juu ya kitu chochote kile; maisha yangu yameharibika. Tumaini alijifunika shuka. Walimsikia akilia kwa kwikwi ndani ya shuka.
>
> John, Tumaini aliita. Anastasia! Mimi si mtu tena kama nyinyi. John mimi sasa ninakufa. Niacheni nife peke yangu. Anastasia! John! Sijui nifanye nini. Sijui nimemkosea nini Mungu! (uk. 97).

Tumaini alitikisa kichwa chake kwa maumivu. Alizungumza tena;

> Anastansia huenda tusionane tena. John kama mimi nikifa, basi usisahau kamwe kumtunza mke wangu mpaka atakapoweza kujikimu mwenyewe. Kuna bado shilingi elfu tatu benkini; elfu mbili mpe Anastasia, elfu moja iliyobaki utamsaidia kujenga nyumba huko nyumbani ili apate mahali pa kuishi.

Anastasia alipoona kuwa Tumaini amekata tamaa na hata anatoa maagizo ya pesa zilizopo na anavyotarajia zitumiwe, naye anampa ujumbe usiotarajiwa.

> Tumaini, nina mtoto wako tumboni mwangu.

Naye tumaini akamjibu;

> Mimi labda sitabahatika kumwona. Nikiwa mimi nimekwenda zangu, basi mtoto huyu utamwita Tabu akiwa msichana. Akiwa mvulana utamwita Matata.
>
> (Uk. 98).

Dondoo hii inaonyesha kuwa Tumaini alijihesabu mfu japo bado alikuwa anapumua na kuongea. Aliona dunia ilifika mwisho kwake.

Dennis anaonekana kukata tamaa pale ambapo anagundua unafiki wa mke wake mama Resi. Vera kwa kawaida alizoea kumwonyesha mumewe mapenzi ya hali ya juu, lakini kumbe alikuwa mzinifu. Mwandishi anaeleza katika uk. 108 kuwa: Dennis aliwasha gari lake na kuelekea nyumbani kwa Tumaini. Mama Resi alianza kujuta kosa lake. Dennis atapata ukweli kutoka kwa Tumaini. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa.

Katika ukurasa wa 110, mwandishi anasisitiza ukataji tamaa wa mama Resi kwa kusema; Hivyo ndiyo mama Resi alivyofuata njia ile ile aliyoipita John. Njia ya Mwanza. Njia ya watu wasiotaka kufanya kazi na kuishi vyema. Mwandishi anafafanua kuwa. Na ndani ya nyumba ya Dennis huo ndio ulikuwa mwisho wa jaribio la utamaduni wa "Kizungu" katika jamii ya "Kiafrika".

Mwisho wa jozi iliyojidai kuwa na mapenzi lakini kwa kutopeana heshima ikaanguka. Kutokana na mfano huu, tunagundua kuwa ndoa kadhaa za kisasa (za wasomi) zinakumbwa na matatizo mengi. Ni ajabu kuona mama Resi akifanya mapenzi na John kwa kitanda kile kile ambacho yeye hulala na mumewe Dennis; na kisha baada ya shughuli hiyo alaghai kwa kuweka mto wenye maandishi "Welcome Back" na kufukiza

marashi ili chumba kinukie na kumvutia mumewe. Wakati mwingine Dennis alipokuja amelewa pombe ya kienyeji, mama Resi alikataa kufanya mapenzi naye kwa kisingizio hicho lakini inaonekana yeye alikuwa anajuwa alichofanya mchana.

Ndoa ya Dennis na mama Resi "ya Kizungu" kamwe hatuwezi kuifananisha na ndoa kati ya Mulele na Bukehele, ile ya Kasala na Mungere. Tabia ya Mungere ni kinyume kabisa na ile ya mama Resi. Katika uk. 5, tunapata maneno haya;

..........Yeye mwenyewe (Mungere) alikuwa hajapata kufahamiana na mwanamume mwingine kijijini isipokuwa Kasala. Tumaini naye alipigwa risasi na kutiwa nguvuni. Alipofikishwa kotini, alikiri makosa yake yote na akahukumiwa kunyongwa.

## 3.5 DHAMIRA YA KIFO KATIKA RIWAYA YA DUNIA UWANJA WA FUJO

Wanaudhanaishi wanaamini kuwa, kifo humuandama binadamu wakati wote wa maisha yake. Kezilahabi anaonekana kukubalina na maneno haya kwa sababu yanadhihirika katika kazi hii.

Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, dhana ya kifo imetawala kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kwanza kabisa, wazazi wa Tumaini mzee Kapinga na Muyango wanaaga dunia. Kwanza kabisa ni mzee Kapinga ambaye anafariki na kumwacha Tumaini chini ya ulinzi wa mamake. Baada ya muda fulani kupita, Muyango naye anaipa dunia kisogo huku akimpa Tumaini wasia unaofaa jinsi atakavyoyaendesha maisha ya baadaye na kwamba akifikia kuoa asiangalie sura bali azingatie tabia.

Musango ambaye alikuwa mpishi wa Tumaini, aliyekuwa anapandwa mabegani na Tumaini kama farasi na Tumaini kurusha mguu wake kama vile anangurumisha pikipiki alifariki muda tu. Bwanake Mugala, babuye Leonila, Dennis, Aurelia, Misana alipatikana ametupwa majini akiwa amefungwa jiwe la shingoni pengine kwa sababu ya tuhuma za kichawi maanake tunamwona bibiye akiwa amerithi tabia hii hatari. Mwisho wa riwaya tunamwona Tumaini anakumbana na mauti yake alipomuua mkuu wa Wilaya kwa kumpiga risasi alipokuwa akiutubia mkutano alipokuwa anahutubia mkutano.

Baada ya mwanadamu kufanya yote duniani, hana budi kuishia kaburini, tena kwa wakati ambao Mungu mwenyewe amehiari.

Wanaudhanaishi wanaamini kuwa, imani ya watu kuwa kifo kinatokea mara moja ni potovu. Kwa hivyo, kulingana na Kezilahabi, tangu mwanadamu anapozaliwa anaanza kufa polepole ingawa yeye anajiona yuko sawa. Mwandishi haoni tofauti kati ya uhai na

kufa, kwani ikiwa ni kwamba tunapoishi tunakufa polepole, basi kufa ni kuishi. Iwapo basi kufa ni kuishi, hakuna mpaka baina ya maisha katika uhai na baada ya kufa. Maoni haya ya Kezilahabi yanaoana na yale ya mwanafalsafa mashuhuri wa mungemeo huu Samuel Beckett ambaye anadai kuwa, maisha ni kuendelea kufa, mfanyiko ambao unaendelea mpaka kiwango kitakiwacho, yaani kifo cha hakika. Kama vile Albert Camus, Kezilahabi hayaoni maisha ya binadamu yakiwa na maana kwani anasema ujasiri wa mwanadamu hukamilishwa na kifo.

## 3.6 MSAKO WA MAANA YA MAISHA KATIKA RIWAYA YA DUNIA UWANJA WA FUJO

Tangu mwanzo wa maisha yake hadi kikomo, mwanadamu daima huwa mbioni akisaka, katika kujuwa na kutafuta maana ya maisha. Yeye hujitahidi kupata furaha na vilevile kupata uhuru wake kama mtu binafsi. Hata hivyo, huku akiendelea na msako huu, anakumbwa na changamoto au hinikizo mbalimbali ambazo zinaathiri kwa kiasi kikubwa mafanikio yake.

Hali ya maisha kukosa maana inasawiriwa katika kazi za Beckett. Mwanadamu hana mwelekeo ulimwenguni; muhimu kwake ni kuzunguka duara lake bila matumaini ya kuona mbele. Kezilahabi anakubaliana na maoni ya wadhanaishi hawa wawili.

Foulquie, P. (1947:56) anafafanua hali hii aliposema:

> Binadamu anaendesha maisha yake katika totoro la usiku kwenye barabara yenye mabonde. Mwingine anaweza kungoja hadi wakati wa mchana, lakini
>
> Ukweli ni kwamba hawezi, kwa vile mchana huo hautafika.

Ukweli kuhusu maisha ya binadamu upo lakini umemkwepa binadamu kokote kule anakoutafuta.

Warnock, M. (1970:78) anaeleza kuwa ukweli upo kwa kila upo kwa kila mtu na ni wajibu wetu kuutafuta.

Katika riwaya hii, tunamuona Dennis anajikakamua vile awezavyo ili kufanikiwa maishani. Baada ya kukumbana na vizuizi asivyotarajia, anasema kuwa anayaona maisha kama fujo za kucheza jukwaani. Baada ya kufanya fujo hizi duniani au jukwaani, yeye

huondoka jukwaani (yaani kuaga dunia) na hivyo kufikia hatima ya mchezo huu wa kuigiza uliokuwa unaendelea duniani. Katika mazungumzo yake na Tumaini mjini, Dennis anaelezea kuwa kuna fujo za aina nyingi. Watu wengine wamefanya fujo zaidi ya wengine. Hao ndio wamejulikana kwa sababu walitumia nguvu. Alitaja majina ya watu wa aina hii kama Napoleon, Juliasi Kaizari, Alekizander, Hitler. Vilevile aliorodhesha wale ambao wamefanya fujo kwa jina la amani na kujulikana, watu kama Bwana Yesu, Linkolin, Livingstone, Gandhi. Alieleza fujo zilizofanywa na waandishi kama Karl Marx, Shakespeare, Plato, Mao na wengine. (Uk. 63).

> Zamani, Dennis alisema, "hata mimi nilifikiri kwamba maisha mazuri sana na kwamba watu wema huenda mbinguni; lakini sasa nina mawazo tofauti kabisa na yale ya zamani. Ulimwengu siku hizi ninauona kama meza – kama meza hii ya kulia unayoiona sasa. Sisi wanadamu ni kama majani. Tunaanguka kutoka juu mtini, tunakuja tunapepea angani kama unyoya namna hii na kuanguka juu ya meza tu! Hakuna atakayerudi juu mtini. Tunao uwezo mdogo wa kutenda mambo na kujipatia furaha angalau kwa sekunde moja. Lakini yote tunayoweza kutenda ukilinganisha na wakati usioweza kushindika ni kama kubeba punje moja ya mchanga kutoka jangwani na kujidai mbele ya ulimwengu.
>
> Zamani nilifikiri kwamba mwanadamu ndiye kiumbe pekee yake mwenye furaha na uhuru. Sasa nimeona kwamba kati ya viumbe mwanadamu ni wa mwisho katika mambo haya mawili. (Uk. 64).

Katika riwaya hii, tunamwona Dennis ambaye alikuwa anafanya kazi akiwa na nafasi nzuri serikalini akiwa amepiga hatua; ana gari nzuri na anaishi kwa nyumba kubwa ya

serikali. Hata hivyo, anapokuwa tayari kuasi ukapera, Vera ambaye alijulikana kwa tabia yake ya kumkubali kila mvulana na hata kubandikwa jina la "Rahisi" Wanapooana na Dennis, ndoa yao inakumbwa na vituko na vitimbi. Yaonekana mama Resi kama alivyojulikana baada ya kumpata kifungua mimba wake Resi, alitamani kuzini na mwanamme yeyote ambaye angefika pale kwake nyumbani lakini kwa bahati mbaya hakuna aliyefika maanake ni kwa mtu mashuhuri serikalini na kwa hivyo wanaume wengine waliogopa. Ndipo tunapomuona akitumia mbinu zote ili kumnasa John mtegoni wa kufanya mapenzi naye John alinaswa akanasika kama samaki aingiaye nyavuni. Urafiki huu unaendelea kwa muda hadi pale Dennis anapojulishwa kuhusu jambo hili na Tumaini. Dennis anaamua kumpa mama Resi talaka na kumrudisha kwao huku akibaki na mtoto wake.

Barua ya pili iliyotoka kwa mama Resi inayomuuliza Dennis kama bado amefikiri Restituta ni mtoto wake inatamausha sana kwa mwanamume ambaye amekuwa akijitahidi kumlea mtoto aliyedhani ni wake kumbe sivyo! Ufichuzi huu ulimfanya Dennis kuudhika sana na kumkasirikia mtoto wake asiye na hatia. Barua ilieleza;

> "Nitakuambia siri moja. Je bado unafikiri Restituta ni mtoto wako? (Uk. 123)

Hii inaonyesha kuwa Vera ambaye tabia yake ya uzinzi iko wazi kabisa, huenda alimpata mtoto huyu na mwanamume mwingine. Dennis aliudhika sana na jambo hili. Kwa mara nyingine alikosa furaha na kuchanganyikiwa zaidi kuhusu maana ya maisha. Mwanzoni alidhania kwamba katika ndoa ataipata furaha kumbe wapi!

Baada ya kumpa Vera Talaka, Dennis anamuoa Bernadeta. Huyu naye alikuwa na "fujo" zake maanake, alipokuwa mjamzito, alimchukia Dennis. Alipata mtoto Bahati na hivyo kuishia kuitwa mama Bahati. Huyu naye alianza kukosana na Dennis siku ile Dennis alikuja saa kumi na moja za usiku. Ilifikia wakati Dennis akampiga kwa sababu ya matusi mazito mazito aliyokuwa anatoa. Isitoshe, kuna wakati mama Bahati alilala chumba cha mazungumzo akajifunika shiti mbili; naye Dennis akalala chumba cha kulala. Mama Bahati alifoka;

> Wewe huwezi kunizidi ujanja Dennis. Tumeona wanaume wangapi, au labda unafikiri wewe ndiye uliyekuwa wa kwanza kuniokota! Kwanza wewe bwege! (uk.21)

Kwa Dennis, tukio hili ni kinyume na matarajio yake ya kupata furaha katika ndoa baada ya ile yake na Vera kutumbukia nyongo. Dennis alikosea maisha maana na akahiari kupatana na mama Bahati maanake aliona akimpa talaka watu watamuelewa kuwa yeye ndiye mwenye makosa. Dennis alisema;

> Ndoa! Ndoa! Ndoa jambo la ajabu! Sijui nifanye nini. Naona maisha yangu hayatatengana kama taabu hii itaendelea kuwa nami. Hivi wanaume wengine pia wana matatizo kama yangu! Mama Resi alikuwa na matatizo yake. Huyu ananipa taabu hizi zote. Je, nimfukuze vile vile? Hapana watu watasema nini juu yangu! Wataniona mimi ndiye mbaya kwa hivyo nitavumilia naye. Lakini mpaka lini? (Uk. 124)

Kulingana na maoni ya mwandishi E. Kezilahabi kuhusu mwanadamu kupata maisha hapa duniani, tukio hili la Dennis linaonyesha bayana kwamba mwanadamu hawezi

kupata furaha hapa duniani pengine kwa sababu anauona ulimwengu kama uwanja wa "fujo". Hili ni jambo ambalo linatamausha na kuondoa matarajio mema aliyonayo mwanadamu katika maisha yake.

Tumaini anaishi katika kijiji cha Bugolola na wazazi wake mpaka pale ambapo wanaaga dunia na kumuachia urithi uliomtia "wazimu" na kupata fursa ya kuchezea maisha ya wasichana. Anaonekana kumtia mimba Leonila na kumkataa huku akisingizia kuwa Leonila alijuwana na wavulana wengi na ni malaya. Tabia hii inaudhi wanakijiji na akaonelea yuko na mambo mawili ya kufanya; arekebishe mwenendo huu, au ahamie mjini. Alihiari kuhamia mjini huku akimtorosha Anastasia na kuhama naye. Jambo hili linatuonyesha kuwa 'fujo' ya mtu binafsi si bora kuliko matakwa ya jamii ya wanabugolola; kwanza jamii ndipo mtu binafsi mambo yake yaje baadaye.

Katika riwaya hii vilevile, tunaona 'fujo' ya Mugala aliyetuhumiwa kuwa mchawi ikikosa kupata kipaumbele dhidi ya fujo ya jamii. Ilimbidi Mugala ahamishwe hadi huko kisima cha wachawi kuliko kuendelea kuwa tishio kwa wanakijiji wapenda amani. Visa hivi viwili, vinatueleza kuwa kamwe mtu binafsi hawezi kufanikiwa katika malengo yake iwapo matakwa ya mtu huyu yanapingana na ya jamii husika. Katika Dunia Uwanja wa Fujo, tuliona familia ya Kasala ikitizama huku wameinamisha vichwa chini bila kufanya lolote, huku akidhihakiwa.

Alipohama mjini, Tumaini anakumbana na changamoto nyingi. Anakutana na Dennis wanaotoka kijiji kimoja ambaye anamkaribisha vizuri na kumfanyia mpango na kupata

kazi ya upelelezi katika mabaa. Kazi hii ndiyo inayomwingiza katika janga kubwa. Mwenye baa anakosa wateja, wanaotoroka wakimwona Tumaini na hivyo anaamua kuunda njama apigwe. Makoroboi, jambazi aliyekuwa na rekodi kadhaa za uhalifu ndiye anayepewa kazi hii, mpango unafanywa ambapo mwanamke mmoja anayeitwa Kristina anamchukuwa Tumaini hadi 'kwake' na hapo ndipo Makoroboi na wenzake wanakuja na kumpiga hadi kuzirai.

Huyu ni Makoroboi yule yule ambaye "fujo" zake za wizi kwa Wanabugolola hazikufua dafu pale alipofukuzwa, kushikwa, kupelekwa kwa mwanangwa na kuhukumiwa. Matakwa yake hayakuwa muhimu kuliko matakwa ya wanakijiji. Wakati huu alikuwa amemaliza kifungo chake.

Alipotoka hospitalini, anaamua kuacha kazi ya upelelezi katika mabaa na kuamua kuwa mkulima maarufu wa pamba. Aliendelea na kufikia ngazi ya kuwaajiri wafanyikazi ishirini ambao aliwalipa shilingi 60/= kwa mwezi. Yeye sasa alikuwa hafanyi kazi; alikuwa amekuwa "Bwana mkubwa". Wengi waliweza kumuita "Mzee" kwa sababu kando na kuotesha kitambi, vilevile alikuwa na gari na hata trekta ya kufanya kazi shambani. Hivyo basi, Tumaini alikuwa miongoni mwa wakwasi wa mjini. Hao ndio walioendeleza ubepari, uchumi na ubinafsi. Wakati huu ndipo Azimio la Arusha lilikuwa limeshika kasi na viongozi wa serikali walijitahidi kwenda vijijini kuelezea siasa hii ya vijiji vya ujamaa ambavyo havikutaka mtu binafsi kujipatia na kufurahia mali wakati wengine wanateseka. Mali ni ya kila mtu na kila mtu ilikuwa ni sharti afanye kazi. Japo

Tumaini alifahamu yote haya, aliyapuuza akidai kuwa yalikuwa ni mambo ya wanasiasa na siasa zao.

Wakati mmoja, kulikuwa na mkutano ambapo mkuu wa serikali alikuja kuelimisha watu kuhusu sera za "vijiji vya ujamaa." Tumaini naye alipata kuhudhuria. Katika maelezo yake, mhutubu anamuita Tumaini na kumtoa mfano kama mtu anayeendeleza ubepari na kumwita mnyonyaji. Mkuu wa wilaya alifafanua:

> Upo unyonyaji wa aina nyingi lakini mfano hiyo miwili inatosha. Lakini wanyonyaji wapo. Kwa mfano mnamwona huyu! Ebu simama bwana watu wakuone! Tumaini alisimama na watu walimzomea. Tumaini alikaa. (Uk. 117).

Tumaini alinung'unika akisema:

> Siwezi kutukanwa na mwanasiasa anayetegemea kura yangu! Haiwezekani! Kuniambia mimi "mnaliona hilo; haya ndiyo manyonyaji haya!" Mimi Tumaini! Mimi sikumkataza kunenepa! Na hata hivyo ninakula jasho langu. Mali niliyoisumbukia mwenyewe wakati watu wengine walipokuwa wakishinda kwenye kangara! Haiwezekani! Potelea mbali vijiji vyao vya vyama ambavyo vimerudisha nyuma maendeleo ya watu wengi. Haiwezekani! (Uk. 120)

Jambo hili lilimuudhi sana Tumaini lakini alizingatia msemo kuwa mwenye nguvu mpishe!

Muda baadaye, Tumaini anapokea waraka kutoka kwa mkuu wa wilaya. Tunawaona watu waliokuja kupimapima shambani kwake, mradi sasa lishachukuliwa na serikali na kugawanywa vijiji vya ujamaa bila yeye kushirikishwa. Kulingana na riwaya hii, hakuna

aliyejali kama alikuwa yuko radhi au hapana, bora serikali ina nguvu na mamlaka ya kuuchukua chochote cha mwananchi, ilimradi serikali ilidai ardhi yote ni yake. Anapoenda kupata ushauri kwa Dennis, anaambiwa:

Siasa mchezo mbaya Tumaini" kama unaona huwezi kabisa kuishi kwenye vijiji vya ujamaa, afadhali chukua mali yako uhamie kabisa mjini. Waachie mashamba wanakijiji. (Uk. 126). Tumaini alijibu;

> Sasa kuna faida gani! Ujamaa ndio mimi sitaki.

Katika mkutano mwingine ulioandaliwa na kuhutubiwa na mkuu wa wilaya, mwanampinduzi na mzalendo hodari, Tumaini ampiga risasi na kumuua mkuu wa wilaya. Alipokuwa anajaribu kutoroka, naye alipigwa risasi na kuanguka chini na kutiwa nguvuni. Alipofikishwa kotini, alikiri makosa yake akahukumiwa kunyongwa.

Dennis anamtembelea Tumaini akiwa gerezani. Tumaini anamkumbusha Dennis yale aliyokuwa amemshauri awali, Tumaini alieleza;

> Ulisema kwamba Dunia Uwanja wa Fujo, kwamba kila mtu lazima atumie kichwa chake ajitahidi, afanye kazi kwa bidii ili apate kujiendeleza. Mimi nimefanya fujo hiyo niweze kuwa tajiri. Lakini sasa niko wapi? (Uk. 129).

Lakini Dennis anajitetea na kumweleza kuwa wakati huo azimio la Arusha lilikuwa halijawa na nguvu. Lakini sasa mambo yamebadilika. Tumaini anakosa maana ya maisha na anamuambia Dennis:

> Dennis sasa nitazame. Nitakufa kama ng'ombe. Nitatupwa pembeni kama gunia zee niliwe na mchwa. (Uk. 129).

Hata hivyo, Dennis alijitahidi kumtia moyo na kumweleza:

> Hapana; wewe ni mtu mwema sana. Lakini umeshindwa kufutilia mbali matakwa ya nafsi kwa manufaa ya umaa.

Ni baada ya kipindi hicho na Dennis ambapo tunamwona mama Tabu na Tabu wakienda kumtembelea Tumaini gerezani. Muda si muda, Tumaini anyongwa kama linavyodhihirisha dondoo hili:

> Simama hapo! Askari alisema. Mbele yake Tumaini aliona bendera ya Taifa ikipepea juu hewani halafu aliona askari wengine. Yule askari aliyemwongoza alimfunika kitambaa cheusi kichwani. Tumaini alishtuka (131).

Kulingana na dondoo hii, ni dhahiri kuwa, matakwa ya mtu binafsi yanapofarikiana na yale ya jamii, mtu binafsi ndiye anayeumia kama tunavyomuona Tumaini. Kulingana na riwaya hii. "fujo" ya jamii au taifa ni muhimu zaidi kuliko "fujo" ya mtu binafsi. Daima mwanadamu huwa yuko mbioni kutafuta furaha, lakini bila mafanikio. (Uk. 113) Tunaelezwa fasiri ya furaha kati ya mazungumzo ya Dennis na Tumaini.

> Dennis, Tumaini alisema tena, unafikiri tumeikaribia furaha? Tumekaribia kupata furaha? Tumaini, furaha ni wazo tu ambalo linaweza kumsukuma mwanadamu mbele ili kumwangamiza ama kumwendeleza lakini mwanadamu hatalishika mkononi.

Kauli hii iliyotolewa na Dennis inatufafanulia kwamba, maisha ni kitu ambacho wanadamu hawapaswi kukitegemea kwa sababu ni "fujo" ya moja kwa moja na kunyima mwanadamu ule uhuru, hiari au furaha anayotarajia. Maisha vilevile yanaonekana ni

adhabu inayoandamana na mateso au maangamizi ambayo huishia katika kifo. Jitihada za mwanadamu za kupata furaha na kuboresha maisha yake huishia kaburini kama tunavyomuona Tumaini.

### 3.7 HITIMISHO

Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, mwandishi amejitahidi kutuonyesha 'fujo' mbalimbali ambazo hutokea katika maisha ya kila siku. Baadhi ya fujo alizozitaja ni umalaya, ulevi, ukatili, ulipizaji kisasi na kadhalika. Tunawaona viruka njia wa Africans' Royal Bar wakifanya kikao cha kuamua ni nani ambaye ataendelea kumnyonya Tumaini mpaka wahakikishe kitita cha hela alichonacho kimeisha. Wanaafikiana na Hadija anakabidhiwa jukumu hili. Anafanikiwa kumfilisi Tumaini, jambo lililomfanya kuamua kuwa mkulima. Fatuma naye aliendelea na John hadi pale John anapofurushwa na Tumaini na kurudi kwao Lutare kwa ajili ya uzembe na utovu wa nidhamu. Hii ni 'fujo' ya aina yake kwa sababu tabia hii inachangia kuvunja ndoa za familia zilizoungana.

Ukatili umetawala katika riwaya hii. Mugala, nyayake Anastasia, anaelezea jinsi mumewe aliuawa; akafungwa jiwe la shingoni na kutoswa majini. Tunaelezwa pia kuwa Kasala alipoenda mjini anakumbana na vijana wanaomwibia nguo na pesa.

Vijana wawili ngomani wanaofumaniwa wakifanya mapenzi katika kichaka ambacho wanaonekana na watu kwa urahisi wanapigwa hadi kufa bila huruma. Hii pia ni 'fujo' ya aina yake.

Makoroboi alifanya 'fujo' kwa kuiba nguo na pesa katika kijiji cha Bugolola. Bila huruma, watu wanamwadhibu kwa kumtukana, kumtemea mate na kumpiga.

Anapopata fursa ya kulipiza kisasi, Makoroboi na wenzake wanampiga Tumaini hadi kuzirai baada ya kupewa pesa na mama Resi na mwenye Africans' Royal Bar.

Ulevi vilevile ni miongoni mwa 'fujo' ambazo zinapatikana katika riwaya hii. Wahusika John, Dennis na Tumaini na wanaume kwa wanawake wanaoishi Bugolola wanaonekana kushiriki kunywa kileo hiki. Kama tunavyoona kupitia kwa Tumaini, ulevi unachangia kuvunja ndoa na kuleta majanga mbalimbali kwa sababu ni baada ya kulewa na Kristina ndipo anaelekezwa kwa nyumba ambamo alikiona cha mtema kuni. 'Fujo' hizi na zingine nyingi kama nilivyoelezea katika sura hii ilichangia sana katika kuteua kichwa cha riwaya hii; *Dunia Uwanja wa Fujo.*

## SURA YA NNE

### 4.1 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Katika sura hii, tumetoa muhtasari wa kazi tuliyofanya huku tukionyesha mambo yaliyojitokeza katika utafiti huu. Hatimaye tumetoa mapendekezo kuhusu utafiti huu.

### 4.2 HITIMISHO

Katika tasnifu hii, tumeshughulikia riwaya mbili za Euphrase Kezilahabi, Kichwamaji, na Dunia Uwanja wa Fujo. Tumetumia nadharia ya udhanaishi katika safari ya uchunguzi wetu. Ni katika kazi hizi ambapo falsafa ya mwandishi huyu kuhusu dhana ya maisha imejiweka bayana. Vilevile, uchunguzi wetu umedhihirisha kuwa mwandishi huyu ni mdhanaishi aliyeathiriwa na wadhanaishi waliomtangulia kama Samuel Becket, Martin Heidegger, Friedrich Nietzsche, Karl Jaspers, Albert Camus na wengineo.

Sura ya pili tumehakiki riwaya ya Kichwamaji tukiegemea mihimili ya udhanaishi ambayo inadhihirisha dhana ya maisha. Tumeona vile ambavyo suala la ukataji tamaa lilivyoangaziwa katika riwaya hii. Kazimoto anaonekana kukata tamaa na kuyakosea maisha maana kwa sababu ya masaibu yaliyomsibu. Kama tunavyoona, matukio haya yanatokea kiusababishi huku yakileta mtiririko na msisimko katika riwaya hii.

Kazimoto anajihusisha na uhusiano wa kimapenzi na viruka njia kama Pili licha ya kwamba ana mke (Sabina). Hulka hii inamfanya aambukizwe ugonjwa wa zinaa. Ni ugonjwa huu ambao umekuwa sababu ya mwanawe kuzaliwa akiwa na kichwa kikubwa

kupita kiasi; jambo linalosababisha kifo chake saa moja baada ya kuzaliwa. Baadaye, anapomtembelea Manase shemejiye, katika mazungumzo yao anatambua asili ya Kichwamaji na hivyo kuamua kuyakatiza maisha yake kwa kujipiga risasi. Anapojiua, anaacha kijikaratasi alichoandika, kufafanua wazo lake kuwa yeye mwenyewe afaa kulaumiwa (anajilaumu) kwa kifo chake mwenyewe kilichotokana na matendo yake. Wote wawili Kazimoto na Manase wanaonekana kukata tamaa pale ambapo wanahofia kuwa kizazi kijacho hakina matumaini yoyote kuhusu tukio la watoto kuja na vichwa vikubwa; kwamba hakuna lolote la maana au la muhimu linalotarajiwa katika vichwa vya aina hii. Wanaonekana kutoa kauli halisi kwa muhtasari wa yale ambayo tunayaona kwa maisha ya sasa, maangamizi yanayotokana na utamaduni wa kizungu na athari za elimu ya kimagharibi.
Kazimoto vilevile anaonekana kukata tamaa baada ya kifo cha dadake Rukia aliyeonekana kuwa na hulka njema lakini kanajisiwa na Manase na kutiwa mimba iliyokuwa sababu ya kifo chake.

Japo Manase ni mtu mashuhuri, aliye na gari na kazi nzuri, tunamwona akiwa amekata tamaa kutokana na changamoto zinazomkabili maishani. Baada ya kujitosa katika ulingo wa anasa, anaambukizwa ugonjwa wa zinaa na mkewe anajikopoa mtoto mwenye kichwa kikubwa. Japo yeye na mkewe Salima wanaishi wakitumia vidonge, wanaishi maisha ya huzuni isiyo na kifani maanake hata Salima anaamua kulichoma gari lao akidai kuwa Manase alilitumia kubebea Malaya. Manase na mkewe wanaishi wakingoja kifo.

Ukengeushi ni suala lingine ambalo tulilitazama katika sura hii. Tumeona kuwa, kuna ukengeushi mara tatu. Wa kwanza ni ukengeushi kati ya vijana na wazee, mtu binafsi na

jamii yake na mtu binafsi na nafsi yake. Tunamwona Kazimoto akiwa mwanafunzi katika chuo kikuu na kuja nyumbani wakati wa likizo. Badala ya kusaidiana shughuli za nyumbani na wazazi wake, yeye anaenda kumtembelea rafikiye Kamata na huko kujiingiza katika tabia ya kulewa pombe na kustarehe na viruka njia. Hivyo akawa amejikengeusha na familia yake. Kazimoto ni shahidi ya kwamba wazee wamejikengeusha na vijana. Kwanza, alishangaa pale ambapo mzee aliingia na fimbo afisini mwa mkuu wa wilaya. Alipoambiwa atoke nje aache fimbo huko kisha arudi, mzee huyu alienda kabisa. Isitoshe, alimuona mzee aliyekuwa mpishi wa Manase na Sabina akijikunyata pale ambapo alikaripiwa na Salima baada ya kuchelewa kuja kazini asubuhi.

Kadhalika, Manase anaonekana kujikengeusha na jamii yake anapodhihirisha kutoukubali utamaduni wake na kuusifu utamaduni wa kizungu. Yote haya ni adhari ya elimu ya magharibi. Rukia anaonyesha ukengeushi mara mbili. Kwanza, kwa masikitiko na simanzi alizokuwa nazo kwa ajili ya mimba aliyotungwa na Manase bila utashi wake; anasusia kula chakula na kuaga dunia akijifungua kwa ajili ya kukosa nguvu. Kwa kifo chake, alijikengeusha na maisha yake mwenyewe.

Uteuzi ni suala lingine linalojitokeza katika riwaya hii. Uteuzi anaofanya kazimoto wa kujihusisha na mapenzi ya kiholela unapelekea kifo cha mwanawe, yeye mwenyewe, na bila shaka yoyote mkewe; japo baadaye. Uteuzi anaofanya Kalia wa kuwanajisi wasichana wa shule na wamama unasababisha kifo chake; baada ya wanakijiji kukerwa na kuchoshwa na vitendo vyake. Ilimradi kulingana na wanaudhanaishi binadamu atawajibikia uteuzi anaofanya.

Tumechunguza kifo katika riwaya hii, kinachoonekana kutawala riwaya hii kuanzia mwanzo hadi mwisho. Safari ya maisha ya binadamu huishia kaburini na hana uwezo wa kubatilisha hali hii. Kwanza ni kifo cha Rukia, mamake Rukia, Kalia, mwanawe Kazimoto na hatimaye Kazimoto mwenyewe. Wanaudhanaishi wanaamini kuwa, maisha ni maumivu ya kusubiri kifo. Tunamwona Manase yu hai lakini anasubiri kifo.

Maisha ya mwanadamu yamekumbwa na hofu, kihoro na wasiwasi. Familia ya Kazimoto daima iliishi kwa wasiwasi na walikuwa hawalali kwa sababu ya watu fulani waliokuwa wakirusha mchanga nyumbani kwao usiku. Familia ya Kabenga walifanya hila ili kuwatishia waingiwe na hofu ili wahamie kijiji kingine. Kazimoto vilevile anaonekana kuishi kwa hofu.

Kadhalika tulilichunguza suala la msako wa maana ya maisha. Wanaudhanaishi wanaamini kuwa, hakuna furaha katika maisha ya binadamu na kwamba kila furaha ina kinyume chake. Binadamu anaonekana kutokuwa na uwezo wa kuyadhibiti maisha. Kazimoto aliona maisha yakiwa ni kitendawili kisichoweza kuteguka hasa baada ya kifo cha Rukia. Alikuwa mzima, hakuwa mgonjwa, lakini afa huku akijifungua. Kazimoto aliona kuwa adhabu kubwa ya mwanadamu yalikuwa ni maisha yenyewe. Katika mazungumzo baina ya Manase na Kazimoto, tunaona Manase akitowa mfano mbalimbali inayoakisi vile mwanadamu yumo mbioni kupata furaha katika maisha bila mafanikio.

Tumehitimisha sura hii kwa kuona mawazo ya wanaudhanaishi kuhusu kuwepo au kutokuwepo kwa Mungu. Kulingana nao, suala hili hawalishughulikii kwa sababu halioani na mantiki ya fikra zao. Tunamuona Kazimoto akifa moyo wa kuendelea kuishi

na kuwaza na kuwazua kwa sababu aliona kuwa kama Mungu alikuwapo, hakuona kwa nini aliweza kufanya ukatili mkubwa kama huo wa kufiliwa na mtotowe, baada ya kazi na taabu waliyopata.

Katika sura ya tatu, tumechanganua riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo. Tumehakiki dhana ya maisha katika riwaya hii huku tukizingatia mihimili husika. Suala la uteuzi linajitokeza bayana katika riwaya hii. Tumaini ambaye kaachiwa kitita cha pesa na mali mengine na wazazi wake anatumia hela hizo kujiingiza katika kuponda mali huku akishiriki ulevi na kufanya mapenzi na wasichana; kilele cha hulka hii ni pale anapomweka mimba Leonila. Jambo hili linamfanya aandamwe na mamake Leonila ili aeleze yaliyotokea. Anatorokea mjini bila ya kumuoa Leonila na kumwacha Leonila na mtotowe kijijini wakiteseka. Baadaye, tunamwona Tumaini akizongwa na matatizo yasiyopimika kule mjini; pengine kwa shauri ya malaika wa Mungu aliyemuacha ilhali alikuwa na uwezo wa kumlea. Isitoshe, Tumaini alijinaki akisema kuwa hakuwa anamhitaji mtoto huyu na kwamba akizaliwa wamtupie mbwa.

Kasala anajutia uteuzi aliofanya wa kumkaripia mamaye Mugala kwa tuhuma kuwa yeye ndiye aliyewaharibu wakina Leonila na Aurelia. Mugala alipewa ugoro na Tumaini ili aendelee na urafiki na Leonila. Baada ya tukio hilo, Mugala anapotea na hivyo kamfanya Kasala kuwa na tumbo joto, hasa pale alipoona nguo ya Mugala ikielea juu ya maji.

Alipokuwa hatarini, huku akifukuzwa na umati wa watu ulioghadhabishwa na tabia yake ya wizi, Makoroboi alimsihi tumaini asifichue mahali alipokuwa. Tumaini kwa upande wake alipuuza ombi hili jambo lililosababisha Makoroboi kula kichapo na kufungwa.

Baada ya kutumika na kutoka gerezani, tunamwona Makoroboi akilipiza kisasi pale aanapopewa pesa na mwenye baa ya Africans' Royal Bar na mama Resi ili amtandike Tumaini. Hivyo basi, Tumaini alifaa kujutia uteuzi aliofanya.

Uteuzi aliofanya Anastasia wa kutorokea mjini akikwepa ndoa ya lazima na mzee Tembo unamfanya ayaone asiyotarajia. Katika vurumai iliyojiri baada ya Khadija kuja nyumbani na kutaka kujuwa sababu zilizomfanya Tumaini asifike kwake zinampa funzo la kukumbuka. Alipohiari kumtandika Hadija na ukuni, Hadija anatoa bastola na Anastasia anaonekana akigaragara chini; naye Tumaini asiweze kumsaidia. Hadija mara ile kugeuka 'mume' akawaamuru alivyotaka na kuwaibia akiba ndogo ya hela walizokuwa nazo.

Ukengeushi vilevile umetajwa katika riwaya hii. Anastasia alijikengeusha na familia yake alipohamia mjini na Tumaini. Anaonekana akiwaza juu ya rafiki zake Leonila na Aurelia maanake sasa katengana nao kwa muda. Kadhalika, mzee Kapinga anaonekana kutoshirikiana na wanakijiji wakati wa uhai wake. Alipofariki, watu wachache mno wanahudhuria mazishi. Ukengeushi uliomwadhiri mzee Kapinga unaathiri hali ya uombolezaji wakati wa kifo chake.

Ukengeushi unadhihirika katika ndoa za kisasa; ndoa za wasomi. Wasomi hawa wanaonekana kufumbata elimu ya kimagharibi, unaleta matukio yasiyotarajiwa. Mama Resi amuambia Mumewe Dennis kuwa amechoka na safari na hivyo kumhitaji Dennis aingie mekoni ili atayarishie wageni chakula. Huku ni kukengeuka na mila na itikadi za jamii za Waafrika.

Kihoro, hofu na dukuduku inaonekana kukumba wapanga njama wa kupigwa kwa Tumaini. Katika mkutano huo, mwenye baa ya Africans' Royal Bar mama Resi na Makoroboi wanahisi kuwa njama yao imetibuka na huenda wakanaswa wakati wowote. Jambo hili lilifanya Makoroboi na wenzake kuhiari kuhamia nchi za mbali kwa kipindi cha miaka miwili. Kwa upande wake, mama Resi ambaye alitarajia Tumaini angeuwawa aliamua kuenda guu kwa guu hadi kwa Tumaini ili amuuwe kwa kisu ndio maana pasiwe na ushahidi lakini anashindwa kufaulu.

Kutofaulu huku kulimfanya aingiwe na hofu zaidi kuwa pengine Dennis angeenda kwa Tumaini kutaka kujuwa ukweli naye Tumaini alifichua siri hii ya uhusiano wa John na Vera iliyoishia kwa talaka.

Mwandishi anatuonyesha ukataji tamaa wa wahusika. Mzee Tembo anakata tamaa baada ya kumkosa Anastasia aliyetoroshwa na Tumaini. Sherehe kubwa ilikuwa imeandaliwa, harusi ya kukata na shoka lakini haikuwa. Tumaini anakata tamaa akiwa hospitalini na majeraha mengi yaliyosababisha yeye kuharibiwa sura baada ya kupigwa na Makoroboi na kundi lake. Anamuagiza John amtunze mke wake mpaka atakapoweza kujikimu mwenyewe. Anaonekana kuagiza mke wake Anastasia amwite mtoto atakayezaliwa Tabu au Matata. Majina hayo mawili ambayo ni ya kimajazi, ni chaguo la Tumaini kulingana na yale aliyokuwa ameyapitia.

Kifo kinaonekana kutawala katika riwaya hii. Wazazi wa Tumaini mzee Kapinga na Muyango wanaaga dunia. Kadhalika, mwandishi ametaja kifo cha mpishi wa akina

Tumaini Musango na mume wa Mugala aliyepatikana ametupwa majini akiwa amefungwa jiwe la shingoni.

Msako wa maana ya maisha unaelezewa katika riwaya hii. Tunaelezwa kuwa, kila mwanadamu huja hapa duniani kwa kipindi chake, akifanya 'fujo' fulani alafu aondoke huku nyuma akiacha wengine waendelee. Tofauti ni kwamba wengine hufanya fujo kubwa kuliko wengine. Anawataja waliofanya fujo kubwa kama Juliasi Kaizari, Hitler, Alekizander, Napoleon n.k. Tunamuona Dennis akitafuta furaha maishani kwa kumuoa Vera. Hata hivyo, furaha hii inatumbukia nyongo pale ambapo anagunduwa kuwa Vera ana uhusiano wa kimapenzi na John. Baada ya kumpa Vera talaka, Dennis anamuoa Bernadeta (mama Bahati) ambaye vilevile anamkosesha raha kwa kumtusi matusi mazito mazito bila kumheshimu.

Baada ya kufilisika, Tumaini alikata shauri kuwa mkulima. Alijitahidi sana na kuwa na wafanyikazi, trekta na kuwa tajiri. Bidii zake ziliambulia patupu kufuatia Azimio la Arusha. Vijiji vya ujamaa vilitarajia watu wote wafanye kazi pamoja na mali iliyoko ni mali ya mwanakijiji. Aliaibishwa na mkuu wa wilaya na kuitwa mnyonyaji. Katika mkutano uliofuata Tumaini ampiga risasi mkuu wa wilaya na kumuua. Anatiwa nguvuni na kuhukumiwa kunyongwa.

## 4.3 MAPENDEKEZO

Uhakiki wetu ulijikita katika nadharia ya udhanaishi. Tunapendekeza kuwa, wahakiki wengine wazihakiki riwaya hizi mbili wakitumia nadharia zingine.

Vilevile, tunapendekeza pafanywe uchunguzi wa fani katika riwaya hizi mbili. Uchunguzi wa fani utaweza kuonyesha vile mwandishi anavyoteua maneno yake kuwasilisha ujumbe wake kwa wasomaji wake.

## MAREJELEO


Baldick, C. (1990), *Oxford Concise Dictionary of Literary Terms:* Oxford. Oxford University press.

Barret, W (1962), *Irrational Man, a Study in Existential Philosophy,* New York. Double Day and Company, Inc Garden City.

Baru T.W. (1992), Bonde la Wakati Katika Riwaya za Kezilahabi. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

*Cassels Encyclopedia of World Literature* (1953), London. Cassels and Company Ltd.

Collins, J. (1968), *The Existentialists:* Chicago. Henry Regenery Company.

Denton D.E. (1974), *Existentialism and Phenomenology in Education,* Collected Essays, New York and London.Teachers College Press.

*Encyclopedia Americana Corporation (1977) Encyclopedia Americana.* New York. Grolier ltd.

*Encyclopedia Britanica* (1958), 15th Impression. Chicago, University of Chicago.

Foulquie, P. (1947), *Existentialism,* London. Dennis Dobson Ltd.

Gatare J.K. (1993), *Dini katika Riwaya za Kezilahabi*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Greene, N.N. (1960), Jean – Paul Sartre; *The Existentialist Ethic*. U.S.A. The University of Michigan Press.

Heinemann, F.H. (1958), *Existentialism and the Modern Predicament*. New York. Harper and Brothers.

Kezilahabi E. (2005). *Rosa Mistika*. Nairobi. KLB.

_____________ (2007), *Dunia Uwanja wa Fujo*. Vide-Muwa Publishers Nairobi.

____________ (2008), *Kichwamaji.* Vide – Muwa Publishers. Nairobi.

Lugano R.S. (1989), *Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mayaka, G (1991), *Ukengeushi wa Wasomi katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi.* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mbatia, M. (2001), Kamusi ya Fasihi. Nairobi. Standand Texbooks Graphics & Publishers.

Morris, V.C. (1966), *Existentialism in Educatio,* New York, Evanson and London. Harper and Row.

Munga, C.I. (1999), *Dhana ya Maisha katika Novela mbili za Euphrase Kezilahabi: Nagona na Mzingile.* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Musau P.M. (1985), *Euphrase Kezilahabi, Mwandishi aliyekata Tamaa.* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Nguku, K.A (2006), *Udhanaishi na Fumbo la Mungu*: Uchanganuzi – Linganishi wa Kichwamaji (Euphrase, Kezilahabi) na la Peste (Albert Camus). (Haijachapishwa).

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999), *Ufundishaji wa Fasihi.* Nairobi. J.K.F.

Njogu, K. & Wafula R. M. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi JKF.

Nkonge, G.K. (2006), *Athari za Udhanaishi katika Kichwamaji na Nguvu ya Sala.* Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Onyango C. F (1993), *The Agnostic Implication of Jean Paul Sartre's Philosophy.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Oxford Advanced Learners Dictionary (1989). London.*Oxford University Press.*

Pojman, Louis P. (1976), *Faith and Reason in the Thought of Kierkegard.* Oxford Bodleian Library. Tasnifu PhD. (Haijachapishwa).

Roubiczek, P. (1964), *Existentialism for and Against.* London. Cambridge University Press.

Shaw, H. (1972), *A Dictionary of Literary Terms.* New York. U.S.A. *Mc Graw-Hill Book Company.*

Tuki (1981), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi. Oxford University Press.

Warnock, M. (1970), *Existentialis,.* London. Oxford University Press.

Wamitila, K.W. (2002) Uhakiki wa Fasihi, Msingi na Vipengele. Nairobi. Phoenix Publishers Ltd.

____________ (2003), Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia, Nairobi. Focus Books.